# TOFAUTI ZA SENTENSI ZA LAHAJA YA KIPEMBA NA KISWAHILI SANIFU ZINAVYOKWAMISHA MAWASILIANO FANISI BAINA YA WAZUNGUMZAJI WA KISWAHILI

**SAIDA SAID KHALFAN**

**NESTORY N. Ligembe**

**Tasnifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Kukamilisha Masharti ya Shahada ya Uzamili Katika Isimu ya Kiswahili**

**Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**

**Novemba, 2015**

**TOFAUTI ZA SENTENSI ZA LAHAJA YA KIPEMBA NA KISWAHILI SANIFU ZINAVYOKWAMISHA MAWASILIANO FANISI BAINA YA WAZUNGUMZAJI WA KISWAHILI**

**Saida Said Khalfan**

**Tasnifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Kukamilisha Masharti ya Shahada ya Uzamili Katika Isimu ya Kiswahili**

**Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**

**Novemba, 2015**

## UTHIBITISHO

Aliyetia sahihi hapa chini anathibitisha kuwa amesoma Tasnifu hii iitwayo "**tofauti za sentensi za lahaja ya kipemba na kiswahili sanifu zinavyokwamisha mawasiliano fanisi [baina ya wazungumzaji wa Kiswahili]**" na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya shahada ya uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Sahihi

Dr.Nestory N. Ligembe

(Msimamizi)

Tarehe: 25 OKTOBA, 2015

## TAMKO LA MTAHINIWA

Mimi, **Saida Said Khalfan**, ninathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu asilia, na kwamba haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili au Shahada nyingine yoyote

Saini …………….

Hairuhusiwi kuzalisha, kunakili, wala kusambaza sehemu yoyote ya tasnifu hii kwa namna yoyote bila kibali cha maandishi kutoka kwa Mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

# SHUKURANI

Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima, afya njema na subira katika kipindi chote cha utafiti. Kufanya utafiti si kazi nyepesi hata kidogo, yeyote aliyewahi kufanya utafiti atakubaliana na mimi. Mtu hawezi kufanya utafiti peke yake mpaka apate msaada wa watu mbali mbali, wa hali na mali, kinyume na hivyo unaweza kukatisha njiani usimalize (ukakata tamaa).

Nitakuwa mwizi wa fadhila endapo nitashindwa kutoa shukurani zangu za dhati kwa watu wote walionisaidia kwa njia moja au nyingine katika kukamilisha kazi hii. Hata hivyo haitakuwa jambo jepesi kuwataja watu wote kwa majina kutokana na wingi wao, ila nitawataja wachache tu ili wawe wawakilishi wa wenzao.

Kwanza natoa shukurani zangu za dhati kwa mwalimu wangu na msimamizi wangu Dkt. Nestory N. Ligembe ambaye kwa kiasi kikubwa ndiye aliyeniongoza na kunisaidia tokea niliopowasilisha mada ya utafiti, kuandika pendekezo na kufanya utafiti hadi kufikia uandikaji wa tasnifu hii. Aliniongoza kwa busara kubwa, alinishauri na kunikosoa pale ambapo palihitaji kurekebishwa bila kuchoka. Pamoja na majukumu mingi sana aliyonayo ya kitaaluma, kifamilia, kijamii na kitaifa, alijitahidi sana kutimiza wajibu wake katika kuisimamia kazi hii. Kwa kweli alinipa mwelekeo imara ulionipa mwanga. Pia amenitatulia matatizo mengi ya kiutafiti. Usaidizi na usimamizi wake haumithiliki. Naomba Allah ambariki kwa kumpa afya njema na mafanikio makubwa katika kazi zake zote.

Pia natoa shukran zangu za dhati kwa walimu wote, Maprofesa na Madokta waliotufundisha na wanaoshiriki katika kutoa kozi hii ya MA. Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania. Mwenyezi Mungu awalipe kheri na awape mafanikio mema katika kazi zao zote. Vile vile naishukuru Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, kwa kuniruhusu kuhudhuria masomo ya uzamili.

Si hayo tu bali pia natoa shukurani maalumu kwa mume wangu Bwana Ali Haji Vuai kwa msaada wake mkubwa wa hali na mali, ushauri, uvumilivu pamoja na kuitunza familia wakati wote nikiwa masomoni. Pia ninamshukuru sana ndugu yangu na mwanafunzi wangu Abdallah Suleiman Hamad kwa mchango wake wa kunielekeza na kuniongoza katika kazi hii ya utafiti.

Aidha ninawashukuru wazazi wangu, ndugu zangu pamoja na watoto wangu kutokana na subira yao na uvumilivu katika kipindi hiki cha masomo na katika harakati za kufanya utafiti huu.

## TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa wazazi wangu Bwana Said Khalfan Slim na marehemu mama yangu Bibi Fatma Abdalla Massoud kwa malezi bora waliyonilea mtoto wao na kunipeleka shule kupata elimu. Pia kwa mume wangu Bwana Ali Haji Vuai pamoja na watoto wangu Maryam, Said, Yunus, Ahmad na Ibrahim kwa uvumilivu wao katika kipindi chote cha utafiti.

**YALIYOMO**

UTHIBITISHO ..... ii
TAMKO LA MTAHINIWA..... iii
SHUKURANI ..... iv
TABARUKU ..... vi
YALIYOMO ..... vii
VIFUPISHO..... x
IKISIRI ..... xii
SURA YA KWANZA ..... 1

1.1 Utangulizi wa Jumla
1.2 Usuli wa mada..... 1
1.3 Malengo ya Utafiti ..... 4
1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti..... 5
1.3.2 Malengo Mahususi ..... 5
1.4 Maswali ya Utafiti..... 5
1.5. Umuhimu wa Utafiti ..... 6
1.6 Kiunzi cha Nadharia ..... 8
1.7 Mipaka ya Utafiti ..... 13
1.8. Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake ..... 14
1.9 Muhutasari wa Sura ..... 15
SURA YA PILI..... 16
MAPITIO YA KAZI TANGULIZI ..... 16
2.1 Utangulizi..... 16
2.2 Mapitio ya Kinadharia ..... 16
2.2.1 Mapitio Kuhusu Sentensi za Kiswahili Sanifu..... 16
2.2.2 Mapitio Kuhusu Vijenzi vya Sentensi za Kiswahili Sanifu ..... 21
2.2.3 Mapitio Kuhusu Sentensi za Lahaja ya Kipemba ..... 24
2.2.3.1 Mapitio Kuhusu Lahaja ya Kipemba ..... 24
2.2.3.2 Mapitio Kuhusu Vijenzi vya Sentensi za Lahaja ya Kipemba ..... 25
2.3 Mapitio ya Kisayansi ..... 26
2.4 Muhutasari wa Sura ..... 33
SURA YA TATU ..... 34
NJIA NA MBINU ZA UTAFITI..... 34
3.1 Utangulizi..... 34
3.2 Umbo la Utafiti ..... 34
3.3 Vyanzo vya Data..... 35
3.3.1 Data za Maandishi..... 35
3.3.2 Data za Masimulizi..... 35
3.3.3 Data za Mapitio ya Maandiko..... 36
3.4 Mbinu ya Utafiti..... 36
3.5 Eneo la Utafiti..... 38
3.6 Sampuli na Usampulishaji ..... 40
3.7 Mbinu za Kukusanya Data..... 41
3.7.1 Mbinu ya ushuhudiaji..... 41
3.7.2 Mbinu ya Mahojiano ..... 42
3.7.3 Mbinu ya Maktabani ..... 43

3.8 Aina ya Data Zilizokusanywa ....................................................................44
3.9 Uchambuzi wa Data ......................................................................................44
3.10 Maadili ya Utafiti ........................................................................................46
3.11 Muhutasari wa Sura ....................................................................................46
SURA YA NNE ....................................................................................................47
UWASILISHAJI NA MAJADILIANO YA MATOKEO ...................................47
4.1 Utangulizi ......................................................................................................47
4.2 Miundo ya Sentensi za Kiswahili Sanifu (KS) na Miundo ya Sentensi za Lahaja ya Kipemba ....................................................................................................48
4.2.1 Viambajengo vya Sentensi za Kiswahili ....................................................48
4.2.1.1 Kishazi ......................................................................................................50
4.2.1.2 Kirai ..........................................................................................................53
4.2.1.3 Neno ..........................................................................................................63
4.2.2 Miundo ya Sentensi za Kiswahili Sanifu (KS) ............................................66
4.2.2.1 Sentensi Zenye Miundo Sahili ..................................................................69
4.2.2.2 Sentensi Zenye Miundo Changamani .......................................................71
4.2.2.3 Sentensi Zenye Miundo Ambatani ............................................................74
4.2.3 Miundo ya Sentensi za Lahaja ya Kipemba (KP) .......................................77
4.2.3.1 Sentensi za Kipemba Zenye Miundo Sahili ..............................................78
4.2.3.2 Sentensi za Kipemba Zenye Miundo Changamani ....................................80
4.2.3.3 Sentensi za Kipemba Zenye Miundo Ambatani .........................................84
4.3 Ulinganishaji wa Miundo ya Sentensi za Kiswahili Sanifu (KS) na Sentensi za Lahaja ya Kipemba (KP) na Namna Zinavyokwamisha Mawasiliano Fanisi ...............87
4.3.1 Uwiano baina ya Miundo ya Sentensi za Kiswahili Sanifu na Miundo ya Sentensi za Lahaja ya Kipemba ...........................................................................................87
4.3.1.1 Muundo wa Sentensi Sahili za Lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu .............88
4.3.1.2 Muundo wa Sentensi Changamani za Lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu....88
4.3.1.3 Sentensi Ambatani Zinaundwa na Vishazi Ambatani Viwili au Zaidi .................89
4.3.2 Tofauti Baina ya Miundo ya Sentensi za Kiswahili Sanifu na Miundo ya Sentensi za Lahaja ya Kipemba ...........................................................................................89
4.3.2.1 Kategoria za Kileksika ..............................................................................90
4.3.2.2 Muundo wa Kirai Nomino ........................................................................91
4.3.2.3 Muundo wa Kirai Kitenzi .........................................................................93
4.3.2.4 Tofauti za Jumla Zinazojitokeza kwenye Vipashio Mbalimbali ..........................94
4.4 Athari za Kimawasiliano Zinazotokana na Tofauti Baina ya Miundo ya Sentensi za Kiswahili Sanifu na Miundo ya Sentensi za Lahaja ya Kipemba ..............................97
4.4.1 Kukosekana kwa Maelewano Baina ya Wazungumzaji ...................................97
4.4.2 Kuelewana Vibaya Baina ya Wazungumzaji ...................................................98
4.5 Muhutasari wa Sura .......................................................................................102
SURA YA TANO .................................................................................................103
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ...................................................................103
5.1 Utangulizi .......................................................................................................103
5.2 Hitimisho la Utafiti .........................................................................................103
5.3 Mchango wa Utafiti Huu .................................................................................104
5.4 Mapendekezo Kuhusu Tafiti za Baadaye .........................................................105
5.5 Muhutasari wa Sura .........................................................................................106
MAREJEO ...........................................................................................................107
KIAMBATISHO 1 ................................................................................................111

MWONGOZO WA MASWALI YA HOJAJI KWA WAZEE WA KIPEMBA .........111
KIAMBATISHO 2........................................................................................................113
MWONGOZO WA MASWALI YA HOJAJI KWA VIJANA WA KIPEMBA WANAOISHI MAENEO YA MJINI..........................................................................113

## VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| BAKITA | = | Baraza la Kiswahili la Tanzania (Taifa) |
| BAKIZA | = | Baraza la Kiswahili la Zanzibar |
| E | = | Kielezi |
| H | = | Kihusishi |
| KB | = | Kirai Kibainishi |
| KE | = | Kirai Elezi |
| KH | = | Kirai Kihusishi |
| KN | = | Kirai Nomino |
| KP | = | Lahaja ya Kipemba |
| KS | = | Kiswahili sanifu |
| KT | = | Kirai Tenzi |
| KU | = | Kirai Unganishi |
| KV | = | Kirai Kivumishi |
| N | = | Nomino |
| Ø | = | Alama ya kapa |
| S | = | Sentensi (iliyoshushwa hadhi) |
| T | = | Kitenzi |
| t | = | Kitenzi Kishirikishi |
| Ts | = | Kitenzi kisaidizi |
| U | = | Kiunganishi |
| V | = | Kivumishi |
| W | = | Kiwakilishi |

| | | |
|---|---|---|
| wkt | = | Wakati |
| -----------------> | = | Isomeke kama (Iandikwe kama) |

# IKISIRI

Utafiti ulihusu uchunguzi juu ya **'Tofauti za Sentensi za Lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu Zinavyokwamisha Mawasiliano Fanisi [Baina ya wazungumzaji wa Kiswahili]'**. Sentensi ni kipashio cha juu cha kimuundo chenye maana kamili. Sentensi ni kipashio cha juu cha uzungumzaji katika lugha yoyote iwayo. Wazungumzaji wanaongozwa na kanuni za lugha wanayoitumia. Kanuzi hizo huzizingatia katika kuteua maneno, kupanga mofu ili kuunda maneno, kupanga maneno ili kuunda virai, kupanga virai ili kuunda vishazi na mwisho kupanga vishazi ili kuunda sentensi. Wazungumzaji wa lugha moja wanaweza kufanana katika kufuata taratibu za lugha lakini wakatofautiana katika uteuzi na mpangilio wa vipashio vya lugha yao. Jambo hili linapelekea kuwa na tofauti baina ya wazungumzaji wa lahaja ya Kipemba na wazungumzaji wa Kiswahili sanifu. Hali hii inapojitokeza bila shaka mawasiliano fanisi yanaweza kukosekana.

Data nyingi zilizotumika katika utafiti huu zilikusanywa uwandani. Maeneo tofauti ya kisiwa cha Pemba yalihusishwa. Mbinu tuliyoitumia katika ukusanyaji wa data ilikuwa ni hojaji. Ugawaji wa dodoso uliwahusisha watu wachache sana. Ushuhudiaji pamoja na uzoefu wetu kwa maeneo ya utafiti pamoja na lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu viliturahisishia zoezi la ukusanyaji data na udhibiti wake. Mbinu ya durusu ya maandiko ilitusaidia wakati wa kusoma kazi za waandishi mbalimbali. Data zilikusanywa kwa mwongozo wa nadharia ya makutano na mwachano, na kuchambuliwa kwa  mbinu ya maelezo kwa mwongozo a nadharia ya sarufi muundo virai.

Uchunguzi wetu ulibaini kuwa pamoja na kuwa Kiswahili sanifu na lahaja ya Kipemba ni mitindo ya lugha ya Kiswahili; pamoja na kuwa lahaja ya usanifishaji (Kiswahili sanifu) ni lahaja iliyokuwa ikizungumzwa Unguja Mjini (Kiunguja [cha wakati huo]) ambapo maeneo ya lahaja mbili hizi (lahaja ya Kipemba na lahaja ya Kiunguja [cha wakati huo]) yanakaribiana sana na watu wake wanachanganyika sana kutokana na sababu za kibiashara, kisiasa na kijamii; bado ipo tofauti kubwa baina ya miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba. Tunaamini kuwa hitimisho la utafiti huu linakidhi mahitaji ya kitaaluma kutokana na hoja zilizojengwa juu ya dhana tuliyoichunguza.

## SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.1 Utangulizi wa Jumla

Utafiti huu umechunguza kuhusu "Tofauti za sentensi za lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu zinavyokwamisha mawasiliano fanis baina ya wazungumzaji wa Kiswahili". Malengo mahsusi ya utafiti huu yalikuwa matatu ambayo ni, kubaini miundo ya sentensi za Kiswahili Sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba, kubaini tofauti baina ya miundo ya sentensi za Kiswahili Sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba na kubaini athari za kimawasiliano zitokanazo na tofauti za miundo ya sentensi baina ya lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu.

Utafiti huu umejengwa na sura tano zinazofafanua hatua mbalimbali za utafiti. Sura ya kwanza inatoa taarifa tangulizi za mada ya utafiti. Sura pili inazungumzia mapitio ya kazi tangulizi. Sura tatu inaonyesha njia na mbinu za utafiti zilizotumika. Sura ya nne inahusu uwasilishaji na majadiliano ya matokeo ya utafiti na sura ya tano na ya mwisho inatoa hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

### 1.1 Usuli wa mada

Utafiti huu unahusu Tofauti za Sentensi za Lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu. Wataalamu wengi wakiwemo Besha, 1994; Khamis na Kiango, 2002; Massamba na wenzake, 1999; Habwe na Karanja, 2004; na Matinde, 2012 (tumetaja wachache) wanakubaliana kuwa sentensi ndicho kipashio cha juu kabisa cha kisintaksia. Sintaksia ni taaluma inayojihusisha na uchambuzi wa miundo ya lugha. Vipashio vingine katika

taaluma ya kisintaksia ni neno, kirai na kishazi ambavyo ndivyo vijenzi vya sentensi. Muundo wa msingi wa sentensi unahusisha virai anuai vinavyoshirikiana kama ilivyoelezwa na Chomsky (1957), kuwa sarufi geuzi ya awali inaanza na vipashio vya kisarufi ambavyo vinajumuisha kanuni muunndo virai yaani kanuni za sintaksia zitumiwazo kuchambua viambajenngo vya sentensi. Sentensi katika lugha ina miundo anuai ikiwemo sentensi sahili, sentensi changamani na sentensi ambatani (Massamba na wenzake, 1999; na Rubanza, 2003). Hata hivyo, kazi hii itajikita katika uchambuzi wa miundo ya Sentensi za Kiswahili sanifu na sentensi za lahaja ya Kipemba tu.

Kiswahili ni lugha yenye chimbuko na inayozungumzwa sehemu za mwambao wa Afrika ya Mashariki (BAKIZA, 2010). Baadhi ya wataalamu wa Isimu historia wanasema kuwa Chimbuko la Kiswahili ni milima ya Kameruni huko Afrika ya Kaskazini Magharibi, na baadhi yao wanasema kuwa chimbuko lake ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) (Maganga, 1997).

Lahaja inazungumzwa katika mitindo anuai kutegemea na eneo walilo wazungumzaji. Hivyo, zipo lahaja za Kiswahili zisizopungua ishirini na moja (King'ei, 2010). Baadhi ya lahaja za Kiswahili ni pamoja na Kipemba kinachozungumzwa katika kisiwa cha Pemba, Kitumbatu kinachozungumzwa Kaskazini Unguja hadi katika kisiwa cha Tumbatu (Tumbatu ni kisiwa kidogo kilichopo Unguja), Kimakunduchi (Kikae) kinachozungumzwa Kusini mwa kisiwa cha Unguja, Kimtang'ata kinachozungumzwa Tanga, Kijomvu kinachozungumzwa Kusini mwa Mombasa, Kimvita kinachozungumzwa Mombasa na Kipate kinachozungumzwa kisiwani Pate. Lahaja zingine ni Kibajuni kinachozungumzwa Kaskazini mwa Mombasa, Kiamu

kinachozungumzwa Lamu, Chi-Miini kinachozungumzwa karibu na mpaka wa Somalia, na Ki-Zwani na Shi-Ngazija zinazozungumzwa visiwani Ngazija, n.k. (King'ei, 2010; Habwe na Karanja, 2004).

Tofauti hii ya uzungumzaji baina ya watumiaji wa eneo moja na lingine huchangia kuwepo vikwazo vya mawasiliano fanisi miongoni mwa baadhi ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili. Hii hutokana na tofauti ya umbali wa kijiografia walionao watumiaji hao (Kipacha 2003). Wakati mwingine, mtumiaji wa Kiswahili wa eneo fulani anaweza kudhaniwa kutotumia Kiswahili kutokana na uzungumzaji wake kuathiriwa zaidi na eneo alipo kiasi cha kutoeleweka kabisa.

Aina ya lugha inayoweza kuwaunganisha watumiaji wote wa lugha ile ile bila kujali tofauti zao za kijiografia na kijamii ni lugha sanifu. Kiswahili Sanifu ndicho kiunganishi cha watumiaji wote wa Kiswahili. Hata hivyo, Kiswahili Sanifu kinaweza kuwa na tofauti kubwa kilinganishwapo na lahaja zake.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Ipo shaka ya kuwa kuna tatizo la kutofanyika mawasiliano fanisi baina ya wazungumzaji wa Kiswahili cha Kipemba na wale wa Kiswahili sanifu (Juma, 2011; Abdalla, 2012). Muundo wa sentensi za lahaja ya Kipemba kinachozungumzwa kwenye baadhi ya maeneo katika kisiwa hicho unatofautiana kwa kiasi kikubwa na ule wa Kiswahili sanifu. Jambo hilo ni moja ya mambo yanayofikiriwa kukwamisha mawasiliano fanisi baina ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili sanifu na

wazungungumzaji wa lahaja ya Kipemba. Mambo mengine yanayokwamisha mwasiliano fanisi baina ya wazungumzaji hawa wa makundi mawili ni kiimbo, lafudhi, kategoria za kileksika, matamshi, ufupishaji wa maneno, na uunganishaji wa maneno. Tofauti baina ya miundo ya sentensi hizo zinadaiwa kuwa chanzo cha mzungumzaji wa Kiswahili ambaye si Mpemba kushindwa kuyaelewa mazungumzo ya wazungumzaji wa lahaja ya Kipemba. Juma (2011) katika utafiti wake juu ya Kipemba cha Wete na Micheweni alionesha kwamba lahaja ya Kipemba inayozungumzwa katika wilaya ya Micheweni ina msamiati wa kipekee inayoweza kusababisha mzungumzaji wa lahaja zingine za Kiswahili na Kiswahili sanifu kushindwa kuwasiliana kwa ufanisi. Pia Abdalla (2012) katika utafiti wake juu ya viangami ndani ya lahaja ya Kipemba alionyesha jinsi vinavyokwamisha mawasiliano fanisi.

Kwa mujibu wa tafsiri za sentensi za watafiti hao (Juma, 2011; Abdalla, 2012) huenda wazungumzaji wa Kiswahili sanifu wasiokua Wapemba au wanaoishi karibu na Wapemba wasengezifahamu sentensi hizo. Hivyo basi wazungumzaji hao wangekosa mawasiliano fanisi. Kwa sababu hiyo utafiti huu ulikusudia kuchunguza tofauti za miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba na sentensi za Kiswahili sanifu na jinsi zinavyokwamisha mawasiliano fanisi baina ya wazungumzaji wa Kiswahili na lahaja zake.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Adam (2008) anaeleza kuwa malengo ya utafiti ni yale madhumuni yaliyokusudiwa na mtafiti. Malengo hutueleza mtafiti anataka kupata nini mwisho wa utafiti wake. Malengo ya utafiti yamegawanyika katika lengo kuu na malengo mahususi.

### 1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti

Kuchunguza tofauti za sentensi za lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu ili kubaini jinsi zinavyokwamisha mawasiliano fanisi baina ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili.

### 1.3.2 Malengo Mahususi

Malengo mahsusi ya utafiti huu yalikuwa;

i) Kubaini miundo ya sentensi za Kiswahili Sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba.

ii) Kubaini tofauti baina ya miundo ya sentensi za Kiswahili Sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba.

iii) Kubaini athari za kimawasiliano zitokanazo na tofauti za miundo ya sentensi baina ya lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

Andrews (2003) anafafanua kuwa maswali ya utafiti hutokana na Malengo ya utafiti. Maandalizi ya maswali haya ni kazi inayohitaji muda wa kutosha, kwa sababu ndio dira ya kufanyia utafiti. Majibu ya maswali ya utafiti yanatakiwa yaongeze maarifa katika taaluma inayofanyiwa utafiti. Kwa sababu hiyo, utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

i). Miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu na Miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba ikoje?

ii). Ni zipi tofauti baina ya miundo ya sentensi za Kiswahili Sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba?

iii). Kwa jinsi gani mawasiliano fanisi huathiriwa na tofauti za miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu?

### 1.5. Umuhimu wa Utafiti

Katika lugha yoyote ile mawasiliano fanisi ni jambo la lazima ili kufikia lengo la mazungumzo. Mawasiliano fanisi hufikiwa pale ambapo taarifa kutoka kwa msemaji au mwandishi itafika na kupokelewa na kufasiliwa na msikilizaji au msomaji. Endapo taarifa ikitoka kwa msemaji au mwandishi itapokelewa lakini haikufasiliwa ilivyokusudiwa na msemaji au mwandishi, basi mawasiliano hayo hayatakuwa fanisi.

Kwa sababu lugha hutumika kwenye nyanja zote za maisha ya binadamu ikiwemo kisiasa, uchumi (maendeleo), kijamii na kiutamaduni; ni dhahiri kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya mawasiliano fanisi na maendeleo katika nyanja mbalimbali zikiwemo za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kitamaduni. Katika maendeleo ya kiuchumi, mawasiliano fanisi huchangia uzalishaji kwenye nyanja mbalimbali kupitia vipindi, mikutano na ushauri au taaluma inayotolewa kwenye maeneo hayo ikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi na nyanja nyingine za uzalishaji.

Kwa upande wa kisiasa, mawasiliano fanisi husaidia ujenzi wa demokrasia kwa kuelimisha jamii juu ya haki na wajibu wa raia, kujenga mshikamano na kuondoa migogoro katika jamii miongoni mwao. Hali hii huipa nafasi jamii kushiriki katika

uzalishaji na kuongeza kasi ya maendeleo. Kwa upande wa kijamii, mawasiliano fanisi huisaidia jamii kuishi kwa maelewano kwa kujihisi kwamba wao ni watu wamoja, wenye utamaduni mmoja hasa ikizingatiwa kwamba lugha ndio nyenzo kuu ya mawasiliano ambayo huwaunganisha watu mbalimbali katika jamii. Tofauti ya mawasiliano ya lugha huakisi tofauti ya utamaduni na matokeo yake wanajamii kujihisi kuwa watu tofauti.

Kwa mantiki hiyo basi mawasiliano fanisi ndio yanayosaidia kuleta maendeleo kwa taifa ambapo wanajamii wote huonekana kama ni watu wa jamii moja wenye utamaduni mmoja kutokana na kuunganishwa na lugha inayowawezesha kuwasiliana kwa ufanisi. Hali hii inaonyesha kwamba kuna haja ya kufanyika utafiti huu ili kuchunguza athari za tofauti za minundo ya sentensi za jamii lugha hizo mbili zinavyokwamisha mawasiliano fanisi baina ya wasemaji wa lugha ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yanategemea kunufaisha makundi mbalimbali ikiwemo serikali, wanaisimu, watafiti na wanajamii kwa ujumla kama ifuatavyo:

Utafiti huu utaongeza maarifa juu ya lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu. Pia utafiti huu utaogeza marejeleo kwa wanaisimu na watafiti wengine. Vilevile unaweza kutoa mwanga wa kuanza kuziangalia upya baadhi ya lahaja za Kiswahili, baadhi yao kama lahaja ya Kipemba huenda ikawa inaanza kujijengea sifa ya kuwa lugha kamili. Aidha, utafiti huu utafungua uwanja wa utafiti kwa maeneo mengine ya kiisimu kwa lahaja ya Kipemba na kuwashawishi wanaisimu kutafiti lahaja nyingine za Kiswahili. Pia, utafiti

huu utawasaidia wakuza mitaala kupanga mitaala ili wanafunzi waelewe kwa undani, juu ya lahaja mbalimbali za Kiswahili na maeneo zinamotumika.

Kwa upande mwengine utafiti huu unategemewa sana kuwanufaisha watunga sera na watekelezaji wa mipango ya maendeleo kuzingatia sana kigezo cha lugha wanapopanga na kutekeleza mipango mbalimbali kwenye jamii zenye utofauti wa lugha. Vile vile, kuihusisha lugha kama moja wapo ya kichocheo cha maendeleo.

Kwa upande wa watunga mitaala utafiti huu unaweza kuwasaidia kufanya maamuzi juu ya matumizi ya lugha na matokeo yake kwenye taaluma. Watunga mitaala wanaweza kuanza kufikiria ama kutumia lugha za wazawa wa eneo husika kufundishia katika ngazi za awali za taaluma au kuweka mkazo maalumu wa kufundisha Kiswahili sanifu ili wanafunzi wa maeneo hayo waweze kukijua vizuri Kiswahili. Lengo ni kuwasaidia kwenye masomo yao na kuanzisha programu za elimu ya awali, ya lazima na ya bure kwenye maeneo hayo.

## 1.6 Kiunzi cha Nadharia

Katika kufikia malengo ya utafiti huu tuliongozwa na nadharia ya makutano na mwachano ya Giles (1982) na Nadharia ya Sarufi Miundo Virai ya Chomsky (1957) ili kubainisha tofauti za miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba na sentensi za Kiswahili sanifu zinavyokwamisha mawasiliano fanisi (baina ya wazungumzaji wa Kiswahili).

Utafiti huu ulitumia nadharia ya **Makutano na Mwachano** ya Giles (1982) wakati wa kukusanya data kwa dhamiri ya kugundua tungo za lahaja ya Kipemba na tungo za Kiswahili Sanifu, kwa kuwa mitindo miwili hii inaingiliana sana kimatumizi katika eneo la utafiti huu.  Aidha, data za utafiti huu zilichambuliwa kwa mwongozo wa nadharia ya **Sarufi Miundo Virai** ili kuona namna virai mbalimbali vinavyopangika katika uundaji wa sentensi za lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu.

Nadharia ya Makutano na Mwachano ya Giles inajaribu kupima mshikamano walionao wanajamii lugha, kuhusu utamaduni wao na lugha yao. Hii ni nadharia ambayo inarejelea dhana ya msambao na mwingiliano wa lugha katika taaluma ya lahaja, na hivyo inaonesha msambao wa lahaja na makutano ya lahaja (Massamba, 2007). Kwa mujibu wa nadharia hii, inapofikia hatua kwa wanajamii-lugha wake kukubali kuacha kutumia lugha yao na kuanza kutumia lugha ya wanajamii nyingine hapo ndipo tunaposema kunakuwa na makutano lakini inapotokea jamii-lugha mbili zinazokaribiana kimaeneo, kila moja ikaendelea kutumia na kudumisha lugha yake basi mazingira kama hayo yanaonesha kwamba kuna mwachano wa jamii lugha hizo (Msanjila na wenzake, 2011).

Kwa mujibu wa King'ei (2010) anasema kuwa kutokana na kuwepo kwa lahaja katika lugha moja, ni wazi kuwa uandishi wa lugha hiyo unaweza kutatanika. Pia, kuwepo kwa lugha nyingi katika jamii kunamaanisha kuwa ipo haja ya kuwa na lugha moja ili itumike kama lugha rasmi. Uteuzi huo wa lugha rasmi uliifanya jamiilugha za Waswahili kuchagua lahaja moja ili itumike kuwaunganisha watu wote

wanaozungumza lugha ya Kiswahili katika mawasiliano. Lahaja iliyochaguliwa na kusanifiwa ni Kiunguja.

Mchakato wa kuchagua lugha ili itumike katika mawasiliano mapana hauna budi utanguliwe na utafiti wa lugha zilizo katika jamii husika kwa kuzingatia vigezo mahsusi. Vigezo hivyo ni pamoja na lugha yenye kutumiwa na watu wengi kuliko lugha nyingine katika eneo husika. Pia, iwe ni lugha iliyo rahisi zaidi kujifunza. Vilevile, iwe lugha ambayo imekwisha kuandikwa kwa kiasi fulani, yaani yawepo machapisho ya kutosha katika lugha hiyo. Tena, iwe ni lugha isiyofungamana na jamii au kabila mojawapo katika nchi husika. Kutokana na sifa hizo hapo juu ndizo zilizopelekea lahaja ya Kiunguja ilichaguliwa na kusanifishwa. Kuchaguliwa kwa lahaja hiyo, kusanifishwa na hatimaye kupewa dhima ya kitaifa na kimataifa haimaanishi kwamba lahaja zingine zisiendelee kuwepo.

Kipacha (2003) anafafanua kuwa msambao wa wazungumzaji na jinsi lugha waitumiayo, inavyobadilika huwa ndio chanzo cha kuzuka tofauti ndogondogo za lugha moja tunazoziita lahaja. Kwa upande mwingine, wanajamii wanaotokana na asili moja na ambao walitengana kwa muda mrefu na kutumia lugha tofauti baadaye lugha zao zikalazimika kuingiliana ama kwa sababu za kiuchumi, biashara au hata kuoana; lugha zao hizo huonekana kuwa kama lugha moja. Katika hali hii hapa tunasema kuwa kuna makutano baina ya lugha mbili. Kwa mujibu wa nadharia hii, inapofikia hatua kwa wanajamii lugha wake kukubali kuacha kutumia lugha ya jamiilugha nyingine hapo ndipo tunaposema kumekuwepo na makutano kwa jamiilugha hizi mbili.

Nadharia ya makutano na mwachano imesaidia kwa kiasi kikubwa kupatikana kwa lahaja na kisha kupatikana kwa Kiswahili sanifu kutokana na usanifishaji wa lahaja moja. Nadharia hii hufasiliwa kulingana na muktadha unaokusudiwa kutumika. Pia, hufanyakazi pale inapotokea jamii moja kutengana na nyingine na kuendelea kutokea mabadiliko ya vipengele kadhaa vya kiisimu na hatimaee kutokea lugha tofauti; baadaye hufikia wakati kila lugha ikazaa lahaja yake (Massamba, 2007).

Nadharia ya **Sarufi Miundo Virai** iliasisiwa na Noam Chomsky mwaka 1957. Nadharia hii ilizuka ili kurekebisha taratibu za sarufi za awali. Mtazamo wa awali wa Sarufi Miundo Virai ulitokana na mapungufu ya mtazamo wa awali wa sarufi muundo ukomo. Sarufi Muundo Ukomo ni aina ya sarufi iliyozalisha sentensi kwa kuanzia kushoto kwenda kulia hatua kwa hatua hadi kufikia mwisho wa sentensi hiyo. Chomsky (1957) aliona kuwa sarufi muundo ukomo inaweza kuunda sentensi sahihi na zisizo sahihi hivyo kuwe na sarufi yenye uwezo wa kuzalisha sentensi toka darajia ya juu hadi darajia ya chini. Sarufi Miundo Virai iwe na seti ya darajia zenye ukomo ambazo zinaundwa katika mazingira yanayotuwezesha kuunda semi kwa kuanza na mfuatano unaoruhusu darajia ya juu na kila darajia ya juu inaelekeza katika darajia inayoifuata chini yake hadi katika darajia ya kiwango cha chini kabisa.

Sarufi Miundo Virai inazipa umuhimu kanuni zinazozalisha vijenzi mbalimbali pamoja na uchambuzi wa viambajengo vya tungo. Huchambua sentensi au tungo kwa kuangalia vijenzi vyake na kuviainisha. Lengo kuu la Sarufi Miundo Virai ni kufafanua makundi

ya kisarufi kwa kuonesha uhusiano kati yake. Sarufi Miundo Virai au Sheria Miundo Virai hujikita katika matumizi ya sheria chache kuzalisha sentensi nyingi zisizo na kikomo, ambazo zina usarufi na hata ambazo hazijawahi kutungwa. Sheria ambazo hutumiwa katika Sarufi Miundo Virai huwa si elekezi bali huonesha na kufafanua viambajengo vya sentensi. Hujikita katika uandikaji upya wa sheria za sarufi ambazo hudhihirisha nafasi na uamilifu wa viambajengo vya sentensi, kuanzia kiambajengo kikubwa (sentensi) hadi kiambajengo kidogo (mofu).

Nadharia ya Sarufi Miundo Virai imefafanuliwa na Massamba na wenzake (1999), Rubanza (2003), Habwe na Karanja (2004), Matinde (2012), na wengineo. Tuchunguze mfano wa sentensi ifuatayo kama ilivyochanganuliwa na Massamba na wenzake (1999):

*Kijana mrefu alifungua dirisha*

Katika utaratibu wa Sarufi Miundo Virai sentensi hii ingechanganuliwa hivi:

| | | | |
|---|---|---|---|
| S -------------------> | KN | | KT> |
| KN ----------------> | N | | V |
| KT -----------------> | T | | KN |
| T -------------------> | W | wkt | T |
| N -------------------> | {Kijana, dirisha} | | |
| V -------------------> | {Mrefu} | | |
| W ------------------> | {a,……………..} | | |
| wkt -----------------> | {li……………..} | | |
| T --------------------> | {fungua} | | |

(Chanzo: Massamba na wenzake, 1999).

Nadharia ya Sarufi Miundo Virai imesaidia sana katika uchanganuzi wa data za utafiti huu. Imetuwezesha kubainisha, kufafanua na kuchanganua miundo ya sentensi za Kiswahili Sanifu na lahaja ya Kipemba. Imetuwezesha kubainisha viambajengo vya sentensi Kiswahili Sanifu na lahaja ya Kipemba. Hivyo, kwa kiasi kikubwa nadharia ya Sarufi Miundo Virai imetuwezesha kuchanganua lengo mahususi la kwanza la utafiti huu lisemalo 'Kubaini miundo ya sentensi za Kiswahili Sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba' na lengo mahususi la pili la utafiti huu lisemalo 'Kubaini tofauti baina ya miundo ya sentensi za Kiswahili Sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba'. Baada ya kufanikisha uchanganuzi wa malengo mawili haya kupitia nadharia ya Sarufi Miundo Virai tumeweza kwa urahisi 'Kubaini athari za kimawasiliano zitokanazo na tofauti za miundo ya sentensi baina ya lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu' ambalo ndilo lengo mahususi la tatu la utafiti huu.

## 1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umechunguza jinsi tofauti za miundo ya sentensi baina ya lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu zinavyokwamisha mawasiliano fanisi baina ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Utafiti ulijihusisha na sentensi sahili, sentensi changamani na sentensi ambatani. Hivyo, ulinganishaji ulifanywa katika kiwango cha sentensi tu ambapo vijenzi vya miundo hii ya sentensi pamoja na tofauti za kategoria za kileksika (maneno au msamiati) ndivyo vilihusishwa.

## 1.8. Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake

Kuna changamoto kadhaa ambazo ziliweza kujitokeza kwenye utafiti huu, baadhi ya changamoto hizo ni:

Tatizo la ukusanyaji wa data: Maneno (kategoria za kileksika) yaliweza kuleta ugumu wa uelewa kwa mtafiti kwa vile mtafiti alishindwa kuelewa kategoria za kileksika za eneo hilo. Hata hivyo, mtafiti alitafuta mtu anayeelewa vyema kilugha cha eneo hilo na Kiswahili sanifu ili amtafsirie kategoria za kileksika asizozielewa.

Tatizo la upatikanaji wa watafitiwa: Wakati wa kukusanya data watafitiwa wengi walikuweko katika shughuli za kimaendeleo. Hivyo, mtafiti alilazimika kutenga muda ambao aliwapata watafitiwa bila shida.

Tatizo la ufinyu wa muda: Kazi ya utafiti ni ngumu na endelevu. Haina kikomo wala kiwango maalumu cha muda. Kutokana na mahitaji ya kitaaluma, kazi hii inapaswa kukamilika katika muda uliopangwa. Jambo hili limekuwa changamoto katika ufanisi wa kazi hii. Ukusanyaji wa data, hasa upatikanaji wa watafitiwa uliathiriwa sana na ufinyu wa muda. Hata hivyo, tuliweza kuwatumia wenyeji wa maeneo tuliyopanga kukusanya data ili watupangie ratiba nzuri itakayotuwezesha kulifanya zoezi letu lifane. Tunashukuru kwamba wenyeji walitupa ushirikiano mkubwa sana wa kuridhisha .

Tatizo la fedha: Pamoja na kuwa kwake tatizo la kitaifa (na hata kimataifa) tunapenda tulibainishe hapa. Utafiti wetu ulihusisha sana maeneo ya vijijini ambako suala la

usafiri na makazi halikuwa jepesi. Tunashukuru kuwa tulipata wenyeji waliotusaidia kujikimu katika shida zote na walitusaidia katika usafiri pia. Vinginevyo, kazi hii ingekuwa ndoto.

### 1.9 Muhutasari wa Sura

Katika sura hii tumeelezea vipengele mbalimbali vinavyotoa taarifa muhimu za utafiti. Vipengele hivyo ni pamoja na usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti. Pamoja na vipengele hivyo pia kuna kiunzi cha nadharia, mipaka ya utafiti na vikwazo vya utafiti pamoja na utatuzi wake.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI

## 2.1 Utangulizi wa Sura

Sura hii ilihusu taarifa zilizoandikwa kuhusu sentensi. Imetalii zaidi kazi zilizotafiti na/au kuandikwa kuhusu dhana ya sentensi na vipashio vyake. Taarifa hizi zilitusaidia katika kubaini namna dhana ya sentensi ilivyoshughulikiwa na wataalamu mbalimbali. Kazi zilizohusu sentensi za Kiswahili sanifu na miundo yake, na sentensi za lahaja ya Kipemba na miundo yake ndizo zilitusaidia kupata mwanga wa kuitafiti mada hii. Mwisho, tumeonesha pengo lililopo baina ya tafiti hizi za awali na utafiti huu.

## 2.2 Mapitio ya Kinadharia

Kipengele hiki kinahusisha maandiko yaliyojikita na kipashio cha kisintaksia [sentensi]. Maandiko haya yameelezea sentensi na miundo yake, viambajengo vya sentensi, aina na sifa za sentensi, na kadhalika.

### 2.2.1 Mapitio Kuhusu Sentensi za Kiswahili Sanifu

Utafiti huu unajihusisha kuchambua lugha kwa kulinganisha na kulinganua miundo ya sentensi na vipashio vinavyounda sentensi hizo. Kwa mantiki hiyo, dhana ya sentensi ndio ajenda kuu inayoangaliwa kwenye utafiti huu.


Kwa mujibu wa Massamba na wenziwe (1999), sentensi ni kipashio kikubwa kabisa cha kimuundo chenye maana kamili. Mpangilio wa maneno katika sentensi unafanywa kwa utaratibu maalumu na sio shaghalabaghala. Neno moja linapoteuliwa hudai

kufuatwa na neno lingine ambalo lina mnasaba nalo. Miundo ya sentensi huhusisha vipashio vingine vidogo kimuundo. Vipashio hivyo ni virai na vishazi. Wanaendelea kusema kwamba muundo wa msingi wa sentensi huwa unahusisha virai tu, na hasa Kirai Nomino na Kirai Kitenzi. Massamba na wenzake (keshatajwa) wamefasili Kirai kuwa ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini ambacho hakina mahusiano ya kiima-kiarifu. Wazo hili lilitupa dira katika kuzichambua sentensi. Tuliweza kubainisha miundo mbalimbali ya sentensi. Hata hivyo, kipashio cha mofu hakikupewa nafasi kubwa na mtaalamu huyu.

Pia, Massamba na wenzake (2009), wanajadili virai katika Kiswahili Sanifu kwa kuonesha kuwa kirai huundwa kutokana na mahusiano maalumu baina ya maneno. Mahusiano huwa ni ya asili katika lugha na hujidhihirisha kisarufi. Muundo wa kirai hukitwa katika neno kuu katika lugha kama vile nomino, vitenzi, vivumishi, vielezi, na hata viunganishi, maneno haya makuu huonesha aina mbalimbali za virai. Kwa mfano, virai vya Kiswahili ni hivi vifuatavyo; Virai Nomino, Virai Vitenzi, Virai Vivumishi, Virai Vielezi na Virai Viunganishi. Kwa kuwa sentensi huundwa na virai mbalimbali, mawazo ya Massamba na wenzake (keshatajwa) ni mwongozo katika uchambuzi wa sentensi za Kiswahili sanifu na sentensi za lahaja ya Kipemba. Isipokuwa, baadhi ya aina za maneno, mfano, kiwakilishi, kihusishi na kihisishi hayadhihiriki wazi wazi katika miundo ya virai hapo juu.

Besha (1994) ameonesha kuwa kati ya maarifa aliyonayo mjua lugha ni pamoja na kujua muundo sahihi wa sentensi za lugha yake. Sentensi ni kipashio changamano sana.


Sentensi ni tungo iliyo kamili kisarufi, isiyotegemea mazingira ya mawasiliano ili kueleweka. Sifa kuu za uchambuzi wa sentensi ni (kubaini) mfuatano wa maneno katika sentensi, uainishaji wa maneno katika makundi, (kubaini) uhusiano wa maneno yanayojenga sentensi, na (kubaini) uhusiano kati ya sentensi. Sentensi inaundwa na sehemu kuu mbili *kundi nomino* na *kundi tenzi.*




(Chanzo: Besha, 1994)

Wazo la Besha (keshatajwa) limesaidia kubaini vipashio vikuu vijengavyo sentensi. Hata hivyo, vipashio hivi vikihusishwa na muundo wa sentensi vitabainika kwenye miundo sahili na miundo changamani pekee. Ama miundo ambatani huhusisha sentensi mbili au zaidi.

Habwe na Karanja (2004) wanafafanua sentensi kama kipashio kinachoshughulikiwa na sintaksia. Upeo wa sintaksia huhusika na uchambuzi wa sentensi na viambajengo vyake kama vile virai na vishazi. Sintaksia pia huhusika na uteuzi na kuchunguza mpangilio na uhusiano wa maneno katika sentensi. Shughuli moja wapo kubwa ya wanaumuundo ilikuwa kuchanganua sentensi kiuambajengo jirani. Yaani, sentensi zilichanganuliwa kwa mujibu wa ujirani wa viambajengo.




(Chanzo: Habwe na Karanja, 2004)

Rubanza (2003) ameandika kuwa sentensi ni tungo iliyo na kifungu nomino na kifungu tenzi. Kifungu nomino kinaweza kuwa kimedondoshwa kiasi cha kuonekana kana kwamba hakipo. Ukamilifu wa sentensi ni kuwa na maana kamili. Sentensi sio mkururo wa maneno yasiyokuwa na muundo. Sentensi huundwa na viambajengo vya darajia tofauti. Darajia hizo ni sauti ambazo husukwa kwa kanuni ya lugha husika na kuunda maneno. Maneno pia kwa utaratibu wa lugha husika yana kanuni ambayo hufuatwa katika kuyaunda na kuyafuatisha ili yaunde virai. Virai huunda sentensi. Wazo hili lilitusaidia katika kuliendea lengo la utafiti huu kwani tuliweza kuigawa sentensi katika darajia za mofu, neno, kirai na kishazi. Isipokuwa, Rubanza (keshatajwa) amegusa sentensi za Kiswahili sanifu pekee pasipo kuzihusisha sentensi za lahaja ya Kipemba.

Khamisi na Kiango (2002) wameifasili sentensi kwa mkabala huo wa sarufi mapokeo, wanasema "*sentensi ni kundi la maneno lenye sehemu kuu mbili: **kiima** na **kiarifu** na ambalo halitegemei au kujitegemeza kwenye kundi jingine la maneno ili kupata maana*

*kamili*". Pia, wametaja aina tatu za sentensi ambazo ni sentensi sahili, sentensi ambatani na sentensi changamano. Ingawa tumeweza kuufahamu muundo wa msingi wa sentensi pamoja na dhima za vipashio vyake; pia, aina za sentensi lakini Khamisi na Kiango (washatajwa) wamejikita kwenye istilahi za kikazi na kuacha istilahi za kimuundo.

Khamis (2011) anaifasili sentensi kuwa "*Tungo sentensi ni tungo ya neno moja au kikundi cha maneno chenye kiima na kiarifu pamoja na kuwa na maana au taarifa inayojitosheleza au maana kamili… hakuna sentensi inayokosa kiima na kiarifu. Sentensi ikikosa kiima na kiarifu basi huwa ni tungo tu bali si sentensi*. Hapa tuliweza kuona vipashio vya lazima kwente sentensi ambavyo ni kiima na kiarifu. Hata hivyo, Khamis (keshatajwa) ametumia istilahi za kikazi katika kubainisha muundo wa sentensi. Aidha, vipashio hivi vinaweza kujitokeza kwenye sentensi sahili na sentensi changamani tu; vipi kuhusu vipashio vinavyounda sentensi ambatani?

Wesana-Chomi (2001; 2003) anazungumzia sentensi kwamba inaweza kufasiliwa kwa kuzingatia kategoria za viambajengo vinavyounda sentensi [KN, V, KT, N, T, TS, KE, E, KH, H, n.k] na kazi zifanywazo na viambajengo vya kikategoria [kiima, kikundi kiarifu, kiarifu, yambwa, yambiwa na chagizo]. Kwa mujibu wa muundo wake wa kikategoria sentensi ni tungo iliyoundwa kwa kishazi kimoja au zaidi. Ufafanuzi wa sentensi kwa mujibu wa Wesana-Chomi (keshatajwa) umetusaidia katika kutambua miundo ya aina mbalimbali za sentensi za Kiswahili sanifu. Hata hivyo, sentensi za lahaja ya Kipemba hakuzigusia hata kidogo katika kazi yake.


### 2.2.2 Mapitio Kuhusu Vijenzi vya Sentensi za Kiswahili Sanifu

Sehemu hii tulionesha mawazo ya wataalamu waliogusia vipashio vinavyounda sentensi za Kiswahili sanifu. Licha ya kubainisha viambajengo vya sentensi kama sehemu ya vipashio vya kimuundo, pia tumechunguza wataalamu waliotumia vipashio vya kikazi katika kuelezea vijenzi vya sentensi.

Khamis (2011) anafafanua dhana ya kijenzi kuwa “kijenzi ni umbo lenye kazi mahsusi za kisarufi katika sentensi. Kazi hiyo hutegemea nafasi kilipo kijenzi hicho katika muundo wa sentensi”. Ametaja kiima, kiarifu, shamirisho, chagizo, kikundi jina, kikundi kiwakilishi, kikundi tenzi, kikundi kielezi, fungujina, fungutenzi. Pamoja na kuwa vijenzi alivyovitaja Khamis (keshatajwa) vinadhihirika ndani ya sentensi, ameshindwa kubainisha namna vijenzi hivi vinavyoweza kutofautiana katika udhihirikaji kutegemea na mkabala uliotumiwa na mchambuzi. Aidha, ni ipi tofauti baina ya kikundi tenzi na fungutenzi; kikundi jina na fungujina? Je, kikundi kiwakilishi kinadhihirika katika muktadha upi?

Wesana-Chomi (2003) anasema kuwa “*muundo wa sentensi ni sentensi sahili. Kila sentensi huundwa kwa sehemu za msingi mbili ambazo pia zinaweza kuwa na visehemu vyake vidogo. Sehemu kuu na ndogo za sentensi hujulikana kama* ***viambajengo vya sentensi****. Viambajengo vya sentensi ndivyo vinavyochangia muundo wa sentensi.* Mfano;

*Wanafunzi wote watafanya kazi shambani kesho*




(Chanzo: Wesana-Chomi, 2003)

Maelezo ya Wesana-Chomi (keshatajwa) yametuongoza katika kuchambua na kuchanganua viambajengo vya sentensi. Isipokuwa, uchanganuzi wake umeishia ngazi ya kirai kwa kuonesha maneno yanayounda virai hivyo. Je, maneno hayana muundo dhahiri katika ngazi ya sentensi?

Habwe na Karanja (2004) anaeleza kuwa viambajengo vya kimsingi vya sentensi ni maneno. Maneno huweza kuunda viambajengo vya viwango vya juu kama *vikundi* na *vishazi* ambavyo ni vidogo kuliko sentensi. Kipashio cha kimsingi katika uchambuzi wa sentensi ni neno. Maneno tofauti hufanya kazi tofauti katika uundaji wa sentensi. Wazo hili ni muhimu kwa sababu limebainisha umuhimu wa neno katika uchambuzi wa sentensi kwamba bila maneno basi hapana sentensi. Hata hivyo, kusema kuwa neno

ndiyo kipashio kidogo cha uchambuzi wa sentensi ni hoja ambayo haikubaliki kwa wanaisimu miundo kwani maneno pia yana miundo yake.

Khamisi na Kiango (2002) wamebainisha elementi za muundo wa sentensi. Wametumia sarufi mapokeo kama mkabala wao wa kiuchambuzi. Elementi walizozitaja hapa ni kiima na kiarifu ambapo ndani yake kuna kijalizo kinachohusisha yambwa na yambiwa. Kimsingi, hizi ni kazi zinazofanywa na vipashio vikubwa vinavyojenga sentensi, yaani virai. Je, maneno hayabainishwi kama vipashio vyenye dhima anuai kwenye sentensi?

Massamba na wenzie (1999) anaeleza kuwa miundo ya sentensi huhusisha vipashio vingine vidogo kimiundo. Vipashio hivyo ni virai na vishazi. Muundo wa msingi wa sentensi huhusisha virai tu, na hasa kirai nomino na kirai tenzi. Pia, Kirai Kivumishi, Kirai Kielezi na kirai kiunganishi. Kuna miundo ya sentensi inayohusisha miundo kadhaa ya msingi iliyounganishwa kwa njia mbalimbali. Miundo hii huitwa vishazi. Ingawaje maelezo haya yametusaidia katika kubaini muundo wa sentensi za Kiswahili sanifu, hayakuweka bayana kuhusu muundo wa sentensi za lahaja ya Kipemba. Aidha, virai havikubainishwa miundo yake na kwamba vipashio vidogo kuliko virai havikutajwa hapa.

Rubanza (2003) anaueleza muundo wa sentensi kuwa kiwango cha chini ni maneno. Katika muundo huo kuna vifungu ambavyo ni viambajengo na vifungu vingine si viambajengo. Viambajengo vya sentensi viko katika darajia tofauti. Msingi wa maelezo

yake ni kuwa sentensi inaundwa na virai vinavyotokana na maneno. Maelezo haya yalitusaidia katika uchanganuzi wa sentensi mbalimbali tulizozitumia katika kazi hii. Kila sentensi tuliweza kuigawa katika virai mbalimbali. Isipokuwa,sentensi ambatani ina muundo unaoanza kwenye idadi ya sentensi mbili au zaidi. Jambo hili halikuelezwa moja kwa moja kwenye mawazo yake. Pia, uchambuzi wake umejikita kwenye sentensi za Kiswahili sanifu tu pasipo kuhusisha sentensi za Lahaja ya Kipemba.

### 2.2.3 Mapitio Kuhusu Sentensi za Lahaja ya Kipemba

Kipengele hiki kimejikita katika maandiko yaliyohusu sentensi za lahaja ya Kipemba. Tumebainisha mawazo ya wataalamu walioandika kuhusu lahaja ya Kipemba. Kuhusu miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba yawezekana haijashughulikiwa vya kutosha na pengine maandiko yake ni machache au hayapo kabisa.

#### 2.2.3.1 Mapitio Kuhusu Lahaja ya Kipemba

Mwansoko (1995) katika Mlacha na Hurskainen (1995) ameandika kuhusu nafasi ya lahaja katika kuendeleza kategoria za kileksika na istilahi za Kiswahili sanifu. Ingawaje lahaja ya Kipemba ameiita Kimwambao, ameweza kubainisha maeneo ya Wete – Pemba na Kwale – Micheweni – Pemba kwamba lahaja hii inatumika. Amebainisha baadhi ya istilahi na kategoria za kileksika vinavyotumika katika maeneo hayo. Isipokuwa, hakuangalia chochote kuhusu sentensi wala viambajengo vya sentensi za lahaja ya Kipemba.

Mgullu (1999) ameandika kuhusu lahaja na kubainisha kuwa lahaja ya Kipemba ni miongoni mwa lahaja za Kiswahili. Hakutoa maelezo yoyote kuhusu lahaja ya Kipemba.

Maganga (1997) ameonesha kuwa lahaja ya Kipemba ni miongoni mwa lahaja za Kusini. Ni vilahaja kadhaa vinavyozungumzwa kisiwani Pemba. Mawazo yake yametusaidia katika kazi hii kwani uteuzi wetu wa maeneo wakilishi wakati wa kukusanya data ulizingatia tofauti zilizopo baina ya wazungumzaji wa lahaja ya Kipemba wa maeneo tofauti. Isipokuwa, hakuandika kipengele chochote cha kimuundo kuhusu lahaja ya Kipemba.

King'ei (2010) amezungumzia lahaja na kuonesha kuwa lahaja ya Kipemba ambayo inazungumzwa kisiwani Pemba ni miongoni mwa lahaja kuu za Kiswahili. Hata hivyo, hakuandika chochote kuhusu kategoria za kileksika au sentensi za lahaja ya Kipemba na viambajengo vyake.

Khamis (2008) katika BAKIZA (2008) amezungumzia lugha ya Waswahili kwa kueleza kuwa lugha ya Waswahili ni Kiswahili chenye kujumuisha Viswahili au lahaja zake 16 ikiwemo lahaja ya Kipemba inayozungumzwa katika kisiwa cha Pemba. Hata hivyo, hakubainisha maneno wala sentensi zinavyotumiwa na wazungumzaji wa lahaja hiyo.

**2.2.3.2 Mapitio Kuhusu Vijenzi vya Sentensi za Lahaja ya Kipemba**

Nyandago (2013) alifanya utafiti juu ya uchaguzi linganishi wa sintaksia ya sentensi sharti ya Kiswahili sanifu na Ekegusii. Aligundua kwamba kishazi sharti cha Kiswahili na Ekegusii vinafanana. Alieleza kuwa vishazi hivi vinapatikana katika kategoria ya

kielezi katika sentensi na kuzidi kufafaua kwamba kishazi sharti cha Kiswahili na Ekegusii vina uamilifu wa kielezi katika muundo wa sentensi. Vinatumika kama vipashio vielezi vinavyofafanua vishazi shurutia, vishazi hutoa maelezo ya hali ya matendo ambayo lazima yatimizwe kwanza, ndipo hali au matendo yanayotajwa na vishazi shurutia yaweze kutekelezwa. Lugha hizi mbili zina sentensi sharti zilizo na miundo ya sentensi changamano.

Tofauti kati ya miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba na sentensi za Kiswahili sanifu si jambo linalobishaniwa kama ilivyo tofauti ya lugha na lahaja zake, kwani liko wazi kwa lugha zote. Baadhi ya tafiti zilizofanywa zimeonesha tofauti ya Kiswahili sanifu na Kipemba kwenye misamiati, fonolojia, mofolojia na kiimbo cha lugha. Mpaka sasa hakuna utafiti unaoonesha tofauti za miundo ya sentensi kati ya Kiswahili sanifu na lahaja ya Kipemba jinsi zinavyokwamisha mawasiliano fanisi baina ya wazungumzaji wa Kiswahili, hili ndilo pengo la kitaaluma ambalo utafiti huu unalishungulikia.

## 2.3 Mapitio ya Kisayansi

Miongoni mwa lahaja zilizotafitiwa ni Kimtang'ata (Whiteley,1959), Kivumba (Lamberd,1957), Chichifundi (Lemberd, 1958), Kinjovu na Kingare (Lamberd,1958) na Kipemba (Whiteley,1958).

Licha ya kuwa lugha ya Kiswahili na lahaja zake ni eneo ambalo halijafanyiwa utafiti sana hasa tofauti kati ya lugha ya Kiswahili sanifu na lahaja ya Kipemba. Hata hivyo wapo wanaisimu wachache ambao wamelichunguza eneo hili ama pekee au kwa

kuilinganisha na lahaja zingine zisizokuwa Kipemba. Tafiti zilizofanywa tokea zama za ukoloni mpaka tafiti za hivi karibu, tafiti nyingi zimejikita kwenye kuchunguza foni na leksia (Maganga, 1991; Khamis, 1982; Juma, 2011). Kwa upande wa tofauti za kisintaksia ni tafiti chache sana zimejikita kuchunguza tofauti ya kisintakisia kati ya lahaja za Kiswahili na kwa kadiri ya mapitio yaliyofanywa na mtafiti hakuna utafiti ulichunguza tofauti za kisintaksia kati ya sentensi za lahaja ya Kipemba na sentensi za Kiswahili sanifu zinavyokwamisha mawasiliano fanisi (baina ya wazungumzaji wa Kiswahili).

Kwa kutumia ushahidi wa kimsamiati Ingrams (1924), analinganisha lahaja mbalimbali za Kiswahili ambazo zinazungumzwa katika visiwa vya Zanzibari. Kazi yake inalinganisha Kiunguja, Kitumbatu, Kimakunduchi na Kipemba. Kuhusu lahaja ya Kipemba anasema: Wapemba wanazungumza lahaja inayoitwa Kipemba ambayo inatofautiana sana na Kihadimu na Kitumbatu.

Utafiti mwingine ulifanywa na Stigand (1915), na Sacleux (1909). Katika utafiti wake Sacleux (keshatajwa) aligundua kwamba Kipemba kina tofauti ambazo yeye aliziita kama lahaja. Katika ugunduzi wake alizitaja lugha tofauti (lahaja ndogo) nne (4) na kuzitaja kama zifuatavyo: Kipemba cha Kusini, Kipemba cha Kivitongoji Mvumoni, Kichake Chake cha Chake na Kimsuka cha Chaleni. Katika kazi yake hiyo anaeleza matumizi ya kiambishi “ki” kinachotumika katika Kipemba badala ya “cha”, kama vile Wapemba kutamka “kyombo kyema” badala ya “chombo chema”.

Stigand (keshatajwa) kwa upande wake anabainisha baadhi ya maneno kwa ujumla, akitoa mifano michache ya lahaja hizo za Kipemba. Anataja matumizi ya maneno kama vile yakwe, "yake", mafya "mafiga" na mwivi "mwizi". Mifano hiyo inadhihirisha kuwepo kwa upekee wa kiusemaji katika lahaja ya Kipemba. Hata hivyo, mifano hiyo haioneshi tofauti za miundo ya sentensi kati ya lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu. Mtafiti mwingine alikuwa ni Whiteley (1958), ambaye kwenye utafiti wake juu ya lahaja ya Kipemba alibainisha misamiati inayotumika katika maeneo mbalimbali katika kisiwa cha Pemba. Kwa mfano:

**Jedwali Na. 1.**

| **PAHALI** | **LAHAJA** | **KISWAHILI SANIFU** |
|---|---|---|
| MICHEWENI | Geleka | Potea |
| TUMBE | Uya | Rudi |
| KIUYU | Kulya | Kula |
| CHOKOCHO | Gea | Tupa |
| MATELE | Hipiki | Nikipika |

Baada ya uhuru (mwishoni mwa karne hiyo ya 20) waliibuka wasomi wazawa kuchangia juhudi zilizofanywa na wageni za kutafiti lahaja za Kiswahili. Baadhi yao ni Temu (1980), Batibo (1982), Khamis (1984), Mshindo (1989), na Maganga (1991). Hawa waliendeleza juhudi zilizoanzishwa na wakaoloni. Kitu kinachojitokeza katika tafiti hizo ni kuwa zilikuwa ni tafiti zilizohusisha lahaja mchanganyiko za Tanzania na nje ya Tanzania na hakukuwa na tafiti mahususi za kulinganisha lahaja za Zanzibari.

Alikuwa ni Maganga (1991) aliyelinganisha lahaja za Kiswahili zinazopatikana katika visiwa vya Zanzibari; Kiswahili Sanifu, Kipemba, Kimakunduchi na Kitumbatu. Hata hivyo, katika utafiti wake alilinganisha mofofonolojia (kategoria za kileksika) za lahaja hizi na kugundua kwamba zipo tofauti za msingi baina yao. Isipokuwa, Maganga hakutoa maelezo yoyote juu ya miundo ya sentensi baina ya lahaja ya Kizanzibari na Kiswahili Sanifu.

Matokeo ya tafiti zilizofanywa juu ya mlingano na utofauti wa lahaja ya Kipemba na lahaja nyingine au Kiswahili, yanatoa majibu mchanganyiko. Wakati matokeo ya tafiti yakionesha kwamba hakuna tofauti ya kifonolojia kati ya Kipemba na lahaja nyingine kwa upande wa leksia hali ni tofauti ambapo tafiti nyingi zilizofanywa zimeonesha kwamba baadhi ya maeneo ya maeneo yanamisamiati tofauti na Kiswahili sanifu.

Kwa mfano katika utafiti wa Polome (1967), juu ya Kiswahili na lahaja zake, alibainisha kuwa Micheweni (Pemba) wanazungumza lahaja ndogo ambayo kwa kiasi fulani inatofautiana na maeneo mengine ya Pemba. Kwa mfano, Micheweni wanatumia **‘k-’** badala ya **‘h-’** katika kiambishi cha ukanushi wa nafsi ya pili au ya tatu umoja. Alihitimisha utafiti wake kwamba katika baadhi ya maeneo ya Kaskazini ya Pemba, kama vile ukanda wa Micheweni-Wingwi lahaja ndogo zimetokea. Kipacha (2003) katika utafiti wake ameeleza kwa ufupi sifa bainifu za kifonolojia ambapo ameonesha kuwa fonimu za Kipemba hazitofautiani sana na zile za Kiswahili sanifu. Hata hivyo kwa upande wa kategoria za kileksika, Kipacha ameonesha orodha za leksimu za Kipemba jinsi zinavyotofautiana na zile za Kiswahili sanifu kama ifuatavyo:

| **Lahaja ya Kipemba** | **Kiswahili Sanifu** |
| --- | --- |
| Zino | Jino |
| Vyaa | Zaa |
| Kyombo | Chombo |
| Singo | Shingo |
| Uka | Nenda |

Kama ilivyo kwa Kipacha (keshatajwa), Temu (1980) naye amegusia lahaja ya Kipemba hasa kwa kuzingatia sauti zake (irabu na konsonanti) na kugundua kuwa hakuna tofauti kubwa kati ya sauti za lahaja ya Kipemba na zile za Kiswahili sanifu. Hata hivyo anasema kuwa tofauti huonekana zaidi katika kiwango cha kategoria za kileksika baina ya lahaja hizo. Kwa mfano, aligundua kuwa kuna tofauti ya matumizi ya irabu, kati ya lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu:

| **Kiswahili Sanifu** | **Kipemba** |
| --- | --- |
| /e/ hesabu | /i/ hisabu |
| /u/ fuata | /Ø/fata |
| /u/ nyuki | /o/ nyoki |

Tofauti na matokeo ya Kipacha, Palome, Temu na Batibo (1982) alipofanya utafiti wa kulinganisha lahaja za Kiswahili za Kusini ya mwambao wa Afrika ya Mashariki aligundua kuwa lahaja zoteza mwambao zinakaribiana zinakaribiana na hakuna matatizo katika kuwasiliana baina ya wazungumzaji wa lahaja zote. Utafiti wake huu

ulilinganisha kategoria za kileksika tu, vipengele vingine vya kisarufi vinavyoundwa na kategoria za kileksika huo kama virai, vishazi, na tofauti za miundo ya sentensi hakuvichunguza. Kukosekana kwa mawasiliano fanisi baina ya wazungumzaji wa Kiswahili kutokana na tofauti baina ya lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu kumewavutia watafiti wengi wa lugha ya Kiswahili. Baadhi ya watafiti hao wameonesha tofauti hizo katika baadhi ya vipengele vya kiisimu kama vile viangami na misamiati lakini hawakuchambua sentensi kwa ujumla wake. Kwa mfano, Abdalla (2012), katika utafiti wake juu ya viangami ndani ya lahaja ya Kipemba alionesha viangami jinsi vinavyokwamisha mawasiliano fanisi si tu kati ya Wapemba na wazungumzaji wengine wa Kiswahili sanifu bali pia ndani ya wazungumzaji wenyewe wa lahaja ya Kipemba wa sehemu moja na sehemu nyingine. Katika utafiti wake, Abdalla (keshatajwa) aliangalia mifano ya sentensi mbalimbali. Kama vile:

(a) *Nkate = o unkugwa = shi* (KP)

Mkate wako umeanguka chini (KS)

(b) *Sijahama = po ta = hiuka henda hivi mara moja kisha hirudi papa apa* (KP)

Sijahama hata siku moja huondoka huenda hivi mara moja kisha hurudi hapahapa (KS)

Kwa mujibu wa tafsiri za sentensi za watafiti hao (Abdalla, 2012; Juma, 2011) huenda wazungumzaji wa Kiswahili sanifu wasiokuwa Wapemba au wanaoishi karibu na Wapemba wasingezifahamu sentensi hizo. Watafiti hawa kama wangaliziacha sentensi

zao hivi hivi kwa mzungumzaji asiyekuwa Mpemba asingeweza kupata mawasiliano fanisi

Pia, Juma (2011), alifanya utafiti kuhusu tofauti za Kiswahili kinachozungumzwa Micheweni na Wete mjini kwa kulinganisha na kulinganua vipengele mbalimbali vya kiisimu vikiwemo matamshi, maumbo ya maneno na maana. Aligundua kuwa Kiswahili kinachozungumzwa Micheweni kimetofautiana sana na Wete na kwamba Kiswahili cha Wete kimeshabihiana sana na Kiswahili sanifu. Hata hivyo katika utafiti wake amejikita sana katika kategoria za kileksika na hakuchunguza miundo ya sentensi.

Pamoja na mpishano wa matokeo ya tafiti hizo (Kipacha, 2003; Temu, Batibo, na Juma) ni dhahiri kwamba hakuna utafiti wowote uliofanywa wa kuangalia tofauti za kisintaksia kati ya lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu. Wataalamu hawa walijaribu kuchunguza baadhi ya vipengele vya kiisimu vikiwemo vipengele vya fonolojia, mofolojia na matamshi na hawakugusia kabisa kipengele cha sintaksia. Hata hivyo mpaka sasa hakuna utafiti unaonyesha tofauti za miundo ya sentensi kati ya lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu na jinsi tofauti hizo zinavyoathiri mawasiliano ambalo ni pengo la kitaaluma. Utafiti huu unakusudia kuziba pengo la eneo hilo la sentensi za lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu.

Ikumbukwe kwamba sentensi ndicho kipashio kikubwa zaidi cha uzungumzaji (lugha), ndicho kinachotoa maana na kwa mantiki hiyo ndio msingi wa ama kufanikiwa au kutofanikiwa kwa mawasiliano. Ufanisi wa mawasiliano unategemea sana ufahamu wa misamiati na maana zake, lafudhi na miundo ya sentensi ni miongoni mwa mambo

mengine muhimu. Na kwamba tumeona baadhi ya tafiti zimefanywa juu ya utofauti wa sauti na misamiati kati ya Kipemba na lahaja zingine; hata hivyo, mpaka sasa hakuna utafiti uliooonesha tofauti za miundo ya sentensi baina ya Kiswahili sanifu na lahaja ya Kipemba na namna utofauti huo unavyoathiri mawasiliano, hili ndilo pengo la kitaaluma ambalo utafiti huu unalishughulikia. Mifano hapa chini inadhihirisha baadhi ya tofauti hizo:

(a) Nkutanoni kwena mijitu (KP)

Mkutanoni kulikuwa na watu wengi (KS)

(b) Sijahama = po ta = hiuka henda hivi mara moja kisha harudi papa apa (KP)

Sijahama hata siku moja huondoka huenda hivi mara moja kisha hurudi hapahapa (KS)

(c) Ng’ombe = we ekufa = wa? (KP)

Ng’ombe wake alikufa wapi? (KS)

## 2.4 Muhutasari wa Sura

Sura hii ilijihusisha na taarifa kuhusu kazi zilizofanywa kuhusiana na mada ya utafiti huu. Kazi hizi zilitusaidia sana katika kufanikisha malengo yetu. Sura hii ina maeneo makubwa mawili: mapitio ya kinadharia  ambayo yanahusisha kazi zilizoandikwa na wataalamu mbalimbali pamoja na au pasipo kuhusisha taarifa za uwandani; na mapitio ya kisayansi  ambayo yanahusisha kazi za kitafiti zinazojengwa na taarifa za uwandani.

# SURA YA TATU

# NJIA NA MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inashughulika na mbinu mbalimbali ambazo zimetumika katika mchakato wa kufanya utafiti. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu hizi: mikabala ya utafiti, usanifu wa utafiti, vyanzo vya data, mbinu za kukusanya data, usampulishaji, eneo la utafiti, maadili ya utafiti, uwasilishaji na uchambuzi wa data. Utafiti huu ni utafiti wa kimaelezo ulikusudia kuelezea tofauti za miundo ya sentensi baina ya Kiswahili sanifu na lahaja ya Kipemba na utafiti huu ulifanyika kwenye kisiwa cha Pemba.

## 3.2 Umbo la Utafiti

Utafiti huu umetumia umbo la kimaelezo.Umbo la kimaelezo ni njia ya kukusanyia data na kuzifanyia uchambuzi kwa njia ya kimaelezo ambapo nambari huwa hazitumiki,(Enon,1999).Hivyo data za utafiti huu zilikusanywa na kuchambuliwa kwa njia za maelezo. Mtafiti alichagua mbinu hii kwasababu aliona itamuwezesha kufikia malengo yake ya utafiti. Mbinu hii ilitumiwa na mtafiti kuzichambua data kwa njia ya maelezo kutegemea malengo mahsusi ya utafiti wake.Umbo la utafiti kwa jina jengine linajulikana kama usanifu wa utafiti yaani Research design. Usanifu wa utafiti ni mchoro au ramani inayoonyesha namna utafiti utakavyofanyika tangu zoezi la kukusanya data,kuchambua data na kuandika ripoti ya utafiti (Rebson, 2007). Katika utafiti huu tumechunguza tofauti ya miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu zinvyokwamisha mawasiliano fanisi baina ya wazungumzaji wa Kiswahili.

### 3.3 Vyanzo vya Data

Data kama alivyotuelekeza Adam (2008) ni vielezo vinavyokubalika ambavyo vinathibitisha ukweli wa matokeo. Zipo data za aina mbili: data za msingi (awali) kama anavyozieleza Kothari (2004) ni zile data ambazo hukusanywa kwa mara ya kwanza. Data za upili: hizi ni zile ambazo zimeshakusanywa, zimeshatumika na zimehifadhiwa (Kothari, amekwishatajwa). Utafiti huu umetumia vyanzo vikuu vitatu vya ukusanyaji wa data. Vyanzo hivyo ni maandishi, masimulizi na mapitio ya maandiko. Tulitumia chanzo cha data zaidi ya kimoja ili kupata data zinazofaa na za kutosha kutoa matokeo bora.

#### 3.3.1 Data za Maandishi

Data hizi zilikusanywa kwa kutumia mahojiano. Mtafiti aliwahoji watafitiwa wakati yuko uwandani katika sehemu zilizoteuliwa ili kupata sentensi za lahaja ya Kipemba. Pia watafitiwa walipewa sentensi za Kiswahili sanifu wazigeuze ziwe katika lahaja ya Kipemba, na sentensi za lahaja ya Kipemba kianchozungumzwa katika maeneo wanamoishi wazigeuze ziwe katika Kiswahili sanifu. Data hizi zimejibu maswali ya utafiti. Data hizi zimenukuliwa kwenye madaftari, na simu ya mkononi ilitumika kwa ajili ya kurikodia taarifa.

#### 3.3.2 Data za Masimulizi

Data simulizi zilipatikana katika kanda zilizochaguliwa. Mtafiti alitembelea sehemu zenye mikusanyiko ya watu kama vile sherehe na misiba, katika vyombo vya usafiri

(boti), mikutanoni, mikahawani, sehemu za kuchezea watoto na baraza za mazungumzo kwa lengo la kusikiliza mazungumzo mbalimbali ili kubaini sentensi za lahaja ya Kipemba. Pia mtafiti alisikiliza historia fupi za vijiji hivyo na hadithi za mapokeo na kurikodi. Data iliyopatikana kwa mbinu hii ilitumika kubainisha sentensi za lahaja ya Kipemba.

### 3.3.3 Data za Mapitio ya Maandiko

Wakati mtafiti anafanya utafiti huu, alitembelea asasi mbalimbali zilizo na kumbukumbu za machapisho ya nyaraka kama vile Makavazi, Maktaba na sehemu nyingine za kuhifadhi nyaraka ili kupata taarifa muhimu zinazohusu mada hii ya utafiti.

## 3.4 Mbinu ya Utafiti

Utafiti huu ulitumia njia ya maelezo. Watafitiwa walifanyiwa mahojianao na majibu ya maswali waliyoyatoa yalirikodiwa kwenye karatasi. Kinyume cha hivyo, watafitiwa walipewa mada za kujadili na majadiliano yao yalirikodiwa au watafitiwa walipewa sentensi za Kiswahili sanifu na baadaye walitakiwa wazigeuze kwenye lahaja zao wanazotumia pasipo kubadili ujumbe (maana) wa sentensi hizo. Mtafiti alitumia njia ya mahojiano, ushuhudiaji na majadiliano ya vikundi kwa lengo maalum. Hivyo mtafiti alichuja aina mbalimbali za sentensi zilizomo kwenye mazungumzo hayo.

Sentensi zilikusanywa katika maeneo ya vijijini na mjini. Vijiji vinne vilihusishwa kwa ajili ya kupata miundo halisi ya sentensi za lahaja ya Kipemba. Tulihusisha eneo moja tu la mjini kwa matarajio ya kupata miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu. Sentensi hizo tulizozikusanya kwenye maeneo hayo tofauti ya kisiwa cha Pemba ziliwekwa


kwenye jozi ya sentensi tano kwa mujibu wa maana inayotolewa kwenye sentensi hizo. Jozi hiyo ilikuwa na sentensi ya Kiswahili sanifu (Kiswahili kinachozungumzwa katika mji wa Wete [Kiwete]), sentensi ya lahaja ya Kipemba cha Kimicheweni, sentensi ya lahaja ya Kipemba cha Kikojani, sentensi ya lahaja ya Kipemba cha Kimuambe na sentensi ya lahaja ya Kipemba cha Kindagoni. Kwa ujumla kila aina ya sentensi ilikuwa na jozi tano zenye sentensi tano kwa kila jozi. Hivyo utafiti huu ulichunguza jozi tano za sentensi sahili, jozi tano za sentensi changamano na jozi tano za sentensi ambatano. Kwa ujumla utafiti ulichunguza jozi kumi na tano zenye jumla ya sentensi sabini na tano. Hata hivyo, baada ya uchunguzi huu, data ziliwasilishwa kwa pamoja kutegemea sifa za kimuundo za jozi hizo za sentensi. Hivyo, makundi makuu mawili ya sentensi ndiyo yaliwasilishwa na kuchanganuliwa kwa kina – yaani sentensi za Kiswahili sanifu na sentensi za lahaja ya Kipemba. Kila kundi hapa liligawanywa katika sentensi sahili, sentensi changamano na sentensi ambatano.

Baada ya kuwekwa kwenye jozi, kila jozi ilichunguzwa ili kuangalia mpangilio wa maneno katika sentensi hizo, jinsi baadhi ya maneno yanavyoachwa au kukwamisha mawasiliano fanisi. Baada ya hapo, sentensi za Kiswahili kinachozungumzwa kwenye maeneo mengine ziliwasilishwa kwa wazungumzaji wa Kiswahili sanifu na kutakiwa waeleze maana wanayoipata kwenye sentensi hizo. Kila muulizwaji alipewa sentensi za maeneo ya lahaja za Kipemba na kuulizwa maana zake au walipewa vipande vilivyorikodiwa vya mazungumzo ya lahaja za Kipemba na kutakiwa waeleze kile walichokifahamu baada ya kusikiliza vipande hivyo. Mtafiti alirikodi kila tafsiri sahihi, tafsiri iliyokosewa na wale walioshindwa kutafsiri kabisa.

### 3.5 Eneo la Utafiti

Pemba ni kisiwa kilichopo katika bahari ya hindi, chenye urefu wa takribani kilomita 65 na upana wa kilomita 23. Kisiwa hiki kipo katika latitudi 5, ambapo kwa upande wa Kusini Mashariki kiko umbali wa takribani kilomita 40 ya kisiwa cha Unguja. Upande wa mashariki kiko karibu na Tanga. Kwa mujibu wa sensa ya 2012 Pemba ina wakazi 406,848; ambapo mkoa wa Kaskazini una wakazi 211,732 na mkoa wa Kusini una wakazi 195,116.

Kazi hii ilijikita kwenye eneo linalosemwa kuwa lina uhifadhi mkubwa wa matumizi ya lahaja ya Kipemba Eneo la kisiwa cha Pemba lililohusishwa ni kisiwa cha Kojani na Micheweni kwa mkoa wa Kaskazini, Pemba; na kwa upande wa Kusini, utafiti ulifanyika katika wilaya ya Chake Chake kijiji cha Ndagoni na Wilaya ya Mkoani katika kijiji cha Mwambe kwa lengo la kukusanya taarifa. Ambazo zitakazo wawezesha wa wazungumzaji wa lahaja ya Kipemba, kutokana na tofauti za kimaeneo ambayo yamesababisha kuzuka kwa vipemba (Mlacha 1995). Katika kazi hii, jamii ya wazungumzaji wa lahaja ya Kipemba imeweza kugawanywa katika maeneo mawili makubwa: Eneo la mjini lenye wazungumzaji wengi zaidi wa Kiswahili sanifu kuliko wazungumzaji wa lahaja ya Kipemba. Yawezekana wazee tu ndio huitumia lahaja ya Kipemba mjini. Kwa upande wa pili wazungumzaji wengi zaidi wa lahaja ya Kipemba (hasa Kipemba halisi) walioko vijijini.




**Ramani Na. 1. Kisiwa cha Pemba**

**Chanzo:** **[http://www.zanzibar-holiday.com/zanzibar_pemba_island.html](http://www.zanzibar-holiday.com/zanzibar_pemba_island.html)**

Kwa kuwa uzungumzaji wa lugha sanifu (Kiswahili sanifu) hauathiriwi na tofauti za kimaeneo, mji wa Wete tumeuteua kama eneo letu la utafiti litakalotuwezesha kupata Kiswahili sanifu. Tuliteua maeneo matatu tunayoamini kuwa yana vikundi vya vijana wanaopenda kukaa pamoja au kushirikiana katika mambo mbalimbali. Maeneo yenyewe ni Bopwe, Utaani na Kipangani. Maeneo mengine ambayo tutakusanya data za uwandani zihusuzo lahaja ya Kipemba tumeyagawa katika kanda nne za kiutafiti: kanda ya kwanza inahusisha eneo la Wilaya ya Micheweni, hapa tumeegemea ukanda wa Kaskazini Mashariki ya kisiwa cha Pemba, katika kijiji cha Micheweni; kanda ya pili inahusisha eneo Wilaya ya Wete, hapa tumeegemea ukanda wa Kaskazini Mashariki ya kisiwa cha Pemba, katika kijiji (kisiwa) cha Kojani; kanda ya tatu inahusisha eneo la Wilaya ya Mkoani, hapa tumeegemea ukanda wa Kusini Mashariki ya kisiwa cha Pemba, katika kijiji cha Mwambe; na kanda ya nne inahusisha eneo la Wilaya ya Chake Chake, hapa tumeegemea ukanda wa Kusini Magharibi mwa kisiwa cha Pemba, katika kijiji cha Ndagoni.

### 3.6 Sampuli na Usampulishaji

Orodho na Kombo (2002) wanafasili sampuli kuwa ni kundi la watu au vitu linaloweza kuhusishwa katika uchunguzi kwa sharti la kuwa na sifa na vigezo linganifu. Usampulishaji ni mchakato wa kuteua idadi fulani ya watu au vitu katika jamii inayofanyiwa utafiti ambao huwakilisha jamii nzima inayofanyiwa utafiti. Katika kuteua sampuli mtafiti huzingatia mada ya utafiti, lengo, muda, gharama, n.k. Utafiti huu ulitumia mbinu ya usampulishaji usio welekeo. Katika mbinu hii uwakilishi hapa hupatikana kwa upendeleo. Mtafiti huamua kumteua muhusika fulani kuwa mwakilishi

kwa sababu binafsi kutegemea na jambo alichunguzalo iwapo tu mwakilishi huyo yumo kwenye kundi la walengwa (wahusika).

Kinadharia, hii ni mbinu ya kuteua wawakilishi kutoka kwenye jamii ya walengwa lakini kiukweli taarifa zinazoweza kupatikana zinaweza kuwa halisi kwa wawakilishi tu wakati jamii iliyoachwa wakati wa uteuzi haina sifa wala data za jambo lichunguzwalo. Linalowezekana hapa ni kuwa wawakilishi na wawakilishwa wanaweza kushirikiana kuwa na **sifa A, B na Ch** lakini mtafiti akadhamiria kuchunguza **sifa D** tu ambayo inamilikiwa na wawakilishi (walioteuliwa) tu. Hivyo, kwa maeneo ya vijijini, mtafiti aliwateua wazee na watoto kwa sababu ndio wanaoaminika kuwa wahifadhi wakubwa wa lahaja ya Kipemba. Katika kila kijiji, mtafiti aliteua wazee watatu (3) kwa ajili ya kufanya nao mahojiano.

## 3.7 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Kuna mbinu nyingi ambazo zilitumika kukusanya taarifa kwenye utafiti huu, baadhi ya mbinu hizo ni kama vile:

### 3.7.1 Mbinu ya ushuhudiaji

Hii ni mbinu ambayo mtafiti amekusanya taarifa kwa kushuhudia na kushiriki katika mazingira halisi. Mtafiti anatakiwa aweke kumbukumbu za taarifa ambazo anazihitaji katika daftari ama sehemu alioiweka makusudi kwa kazi hii. Adam (2008) anasema kuwa matumizi ya mbinu hii ni lazima mtafitiwa awepo kwenye uwanda ili kupata

taarifa kwa usahihi, ni lazima atumie viungo vya hisia ikiwemo kuona kusikia, kugusa, kunusa na kuonja. Ili ushuhudiaji uwe wenye kuleta mafanikio, mtafiti atakuwa makini katika kuandika taarifa, kuvifikia vipengele vyote anavyotaka kuvishuhudia na kuwa na muda wa kutosha. Manufaa ya mbinu hii ni kuwa mtafiti anapata ufahamu wa kina kuhusiana na mada anayoitafiti, pia huielewa vyema jamii anayoifanyia utafiti. Pamoja na hayo, mbinu hii inaweza kuwa na mapungufu ikiwa watafitiwa watajua kuwa wanafuatiliwa wanaweza kufanya mambo tofauti na uhalisia wake. Mbinu hii imeampa fursa mtafiti kuingia darasani na kwenye michezo ya nje.

### 3.7.2 Mbinu ya Mahojiano

Hii ni mbinu ambayo mtafiti anakusanya data akiwa ana kwa ana na mtafitiwa. Mtafiti huuliza maswali na majibu huyarikodi katika daftari la kumbukumbu au kwa kutumia vifaa vya kurikodia kama vile tepu ya kurikodi au simu. Kothari (1990) anaeleza kuwa mbinu hii inahusu mchakato wa kuuliza maswali maswali ambayo hayaeleweki na mtafitiwa. Mtafiti alichagua mbinu hii kwa sababu ina manufaa mengi kama vile kupata fursa ya kufafanua maswali pale ambapo mtafitiwa atakuwa hakufahamu.Pia inatoa fursa ya watafitiwa waliosoma na wasiosoma kushiriki katika kutoa taarifa.Ikiwa mtafiti atajenga mashirikiano mazuri na watafitiwa,hivyo atapata data za uhakika.

Kwa upande mwingine, mbinu hii inaweza kuwa na mapungufu ikiwa mtafiti alilazimisha mtafiti ajibu kama anavyopenda yeye. Vilevile mbinu hii inapoteza muda kwani mtafiti anapaswa kumfuata mtafitiwa katika sehemu yake na asimkute. Mbinu hii ndio iliyotumika kwa kiwango kikubwa kwasababu ilisaidia kuhakiki na

kuthibitisha matokeo ya majibu ya maswali walioulizwa watafitiwa. Mtafitiwa alitakiwa ajibu maswali ya utafiti akiwa peke yake. Hii ilisaidia sana kupata maoni ya moja kwa moja kutoka kwa watafitiwa. Mbinu nyingine ni mahojiano, ni mbinu ambayo inahusisha mazungumzo ya mdomo baina ya mtafiti na mtafitiwa, ambapo mazungumzo hayo yanaweza kuwa uso kwa uso au kwa njia ya simu (Caesar, 2008). Mtafiti aliwahoji wazee 12 ambao aliwateua katika vijiji vinne tulivyovibainisha kuwa vina uhifadhi mkubwa wa matumizi ya lahaja ya Kipemba. Katika kila kijiji tuliteua wazee watatu (3).

Njia nyingine ambayo inaweza kutumika ni makundi ya majadiliano kwa lengo maalumu (Focus Group Discussion). Ni mbinu ambayo mtafiti huandaa mada maalumu anayokusudia ijadiliwe katika kundi ili aweze kunasa majadiliano hayo (Kombo na Tromp, 2006:104). Katika utafiti huu mbinu hii ilitumika kwa lengo la kupata sentensi za Kiswahili sanifu. Mtafiti alifanya mazungumzo na makundi matatu ya vijana wa mitaa (ya mji wa Wete) tuliyoiteua hapo juu. Kiujumla, data za utafiti huu zilikusanywa kwa mbinu mchanganyiko kutegemea na kundi linalohusika katika kutoa data. Mbinu kuu ni Ushuhudiaji, makundi ya majadiliano kwa lengo maalumu na mahojiano.

### 3.7.3 Mbinu ya Maktabani

Maktaba imetumika kwa ajili ya kupata taarifa mbalimbali zinazohusiana na mada hii na maelezo mengine muhimu kuhusiana na utafiti huu. Mtafiti alitaka kuona wataalamu na watafiti wengine wamesema nini kuhusiana na tatizo la utafiti au eneo

linalokaribiana na hilo. Kazi zilizosomwa maktaba zimeweza kuhusiana na nadharia mbalimbali au ufafanuzi wa dhana zinazohusiana na mada.

## 3.8 Aina ya Data Zilizokusanywa

Taarifa zilizokusanywa zinahusu sentensi za Kiswahili sanifu na sentensi za lahaja ya Kipemba kwa ujumla wake. Sentensi hizo zilikuwa ni sentensi sahili, ambatani na changamani katika hali tofauti. Kulikuwa na sentensi zilizoundwa na neno moja tu (Kitenzi) na sentensi zenye maneno ya aina mbalimbali ili kuweza kufanya uchambuzi kwa mawanda mapana zaidi.

## 3.9 Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa taarifa ulihusisha sehemu mbili zenye hatua tofauti. Hatua ya kwanza ilihusu uchambuzi wa tofauti kati ya miundo ya sentensi za Kipemba na Kiswahili sanifu. Na hatua ya pili iliangalia kama tofauti za sentensi zinapelekea wazungumzaji wa Kiswahili sanifu kukosa ufahamu wa Kiswahili kinachozungumzwa na wazungumzaji wa lahaja ya Kipemba.

Ili kuchambua mlingano na tofauti kati ya Kiswahili sanifu na lahaja ya Kipemba na taofauti zinazojitokeza kwa wazungumzaji tofauti wa lahaja yenyewe ya Kipemba, sentensi zenye maana zinazofanana kwa mujibu wa lahaja ya Kipemba na sentensi ya Kiswahili sanifu zilipangwa kwenye jozi moja. Jozi hiyo ilikuwa na sentensi tano. Baadaye mtafiti aliangalia uwiano au utofauti wa vipashio viundavyo sentensi katika jozi hiyo.

Uchunguzi ulifanywa kwenye mpangilio na mfuatano wa maneno katika sentensi hizo, uhusiano wa vipashio vyake katika sentensi kwa kufuata kanuni za kiparadigmatiki na kisintagmatiki. Pia kanuni ya tangamano la irabu kwa sentensi za Kipemba na zile za Kiswahili sanifu lilizingatiwa. Uchunguzi wa mlinganisho na utofauti ulifanywa kwenye mofimu zinazounda maneno yanayotumika kwenye sentensi, mizizi huru na viambishi vinavyotengana na vipashio vingine vinavyojenga sentensi.

Katika kuchunguza kuwa tofauti ya sentensi inaathiri mawasiliano fanisi, sentensi zilizokusanywa kwenye maeneo mbalimbali ya wazungumzaji wa lahaja za Kipemba zililinganishwa na sentensi zilizokusanywa kwa watu ambao wanatumia lugha sanifu.

Majumuisho ya utafiti huu yalifanywa kutokana na mfanano na tofauti kati ya miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu na zile za lahaja ya Kipemba. Hapa tuliangalia mizizi ya maneno na viambishi vyake pamoja na virai na vishazi vinavyounda sentensi hizo. Pia, tuliangalia upeo na kiasi ambacho Wapemba wanaozungumza Kiswahili sanifu walivyoweza au kushindwa kupata maana ya sentensi za lahaja ya Kipemba. Pia, wazungumzaji wa lahaja ya Kipemba wa eneo moja wanavyoweza au kushindwa kufahamu maana za sentensi zinazozungumzwa kwenye maeneo mengine yanayozungumzwa lahaja hiyo hiyo ya Kipemba.

### 3.10 Maadili ya Utafiti

Ili kufanikisha utafiti huu, ni lazima mtafitiwa aelezwe maadili ya utafiti ili aweze kutoa taarifa za ukweli na uhakika (Kombo na Tromp, 2011). Aeker (2002) kama alivyonukuliwa na Adam (2008), "wametaja maadili ya utafiti kuwa ni pamoja na haki ya kuwa na usiri", yaani mtafiti hatatoa siri ya mtafitiwa. Pia ameeleza haki ya mtafitiwa kuhakikishiwa usalama wake, haki ya kujua madhumuni ya utafiti, haki ya kupata matokeo ya utafiti, haki ya kujibu swali takalopenda kujibu na haki ya kukataa kushiriki kwenye utafiti.

Licha ya kuwa taarifa za utafiti huu haziwezi kuleta madhara kwa mtu yeyote,utafiti huu umezingatia misingi yote muhimu ya maadili ikiwemo kupata ridhaa ya wahojiwa na ridhaa ya walezi kwa wahojiwa walio chini ya miaka kumi na nane.Mtafiti aliandika barua ya kuomba ruhusa ya kufanya utafiti katika maeneo husika,sambamba na hilo mtafiti aliomba ridhaa kwa watafitiwa wenyewe.Hivyo utambulisho wa wahojiwa haukuonyeshwa kwa lengo la kuzuia kujuilikana licha ya kuwa kujuilikana kwao hakuna madhara yoyote.

### 3.11 Muhutasari wa Sura

Sura hii ilijikita katika kubainisha mbinu zilizotumika katika utafiti huu. Ilijadili vipengele kadhaa vilivyomwezesha mtafiti kufikia lengo la utafiti huu. Baadhi ya vipengele vya sura hii ni mikabala ya utafiti, usanifu wa utafiti, vyanzo vya data mbinu ya utafiti, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za kukusanya data, aina ya data zilizokusanywa, uchambuzi wa data na maadili ya utafiti.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA MAJADILIANO YA MATOKEO

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha matokeo yaliyopatikana kutokana na utafiti wa uwandani na maktabani na kuyajadili matokeo hayo. Uwasilishaji wa matokeo umefanyika kwa kutumia msingi na kanuni za kiunzi cha nadharia ya makutano na mwachano ya Giles (1982) na Nadharia ya sarufi miundo virai zilitumika ili kubainisha tofauti za miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu na zile za lahaja ya Kipemba zinavyokwamisha mawasiliano fanisi (Baina ya wazungumzaji wa Kiswahili). Uwasilishaji na majadiliano juu ya matokeo hayo umelenga kujibu maswali ya utafiti huu ili kukamilisha malengo ya utafiti. Aidha sura hii inawasilisha matokeo na kuyajadili kwa mujibu wa data iliyochambuliwa na hoja mbalimbali za wanavyuoni kama zilivyo kwenye mapitio ya kazi tangulizi za tasnifu hii.

Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu kama zifuatazo: Sehemu ya kwanza inawasilisha matokeo na kuyajadili kwa kuzingatia miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba (Lengo la [i]); sehemu ya pili inawasilisha na kujadili matokeo yanayohusu tofauti baina ya miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba (Lengo la [ii]); na sehemu ya tatu inawasilisha na kujadili matokeo juu ya athari za kimawasiliano zitokanazo na tofauti za miundo ya sentensi baina ya lahaja ya kipemba na Kiswahili sanifu (Lengo la [iii]).

## 4.2 Miundo ya Sentensi za Kiswahili Sanifu (KS) na Miundo ya Sentensi za Lahaja ya Kipemba

Miundo ya sentensi za lugha za Kibantu inafanana sana. Sentensi zake huundwa na kirai nomino na kirai tenzi. Kirai nomino na kirai tenzi huundwa na viambajengo kadhaa. Viambajengo vya kirai nomino na vile vya kirai tenzi huweza kutofautiana baina ya lugha moja na lugha nyingine (za Kibantu) au lahaja moja na lahaja nyingine (ya lugha ile ile ya Kibantu).

### 4.2.1 Viambajengo vya Sentensi za Kiswahili

Tulieleza hapo awali kuwa sentensi za Kiswahili zinaundwa na vipashio anua'i vinavyobainika katika ngazi tofauti. Mofu hujenga neno, maneno hujenga virai, virai hujenga vishazi na vishazi hujenga sentensi. Inapaswa ieleweke kwamba maelezo haya yalitumika kama msingi wa uchambuzi na ufafanuzi wa nadharia za kimuundo tu kwa sababu katika mazingira halisi, tofauti za kimuundo baina ya mofu, neno, kirai, kishazi na hata sentensi huwa si dhahiri wakati wote. Mfano;


(a) Mama ni chuo bora

(b) Ameruhusiwa

Katika mifano hapo juu kuna sentensi zenye viambajengo tofauti. Sentensi ya (a) imeundwa na kishazi kimoja [Mama ni chuo bora]; virai vitatu ['mama' ni kirai chenye neno moja]; ['ni' ni kirai chenye neno moja]; na ['*ch*uo bora' ni kirai chenye maneno mawili]; maneno ni manne ['mama' ni neno lenye mofu moja], ['ni' ni neno lenye mofu moja]; ['chuo' ni neno lenye mofu mbili] na ['bora' ni neno lenye mofu moja].

Sentensi ya (b) imeundwa na kishazi kimoja pia [ameruhusiwa]; kirai kimoja [ameruhusiwa]; neno moja [ameruhusiwa] na mofu tano [a-me-ruhus-iw-a].

Hoja yetu hapa ni kuwa tofauti za kimuundo baina ya mofu, neno, kirai, kishazi na hata sentensi hazijibainishi katika semi zote zinazotumiwa katika miktadha yote ya uzungumzaji. Yaani, sentensi hazijengwi na vipashio vyenye hadhi sawa kimuundo katika mazungumzo yote. Sentensi ya (a) imeundwa na kipashio 'mama' ambacho kinaweza kuchukuliwa kama mofu [huru], neno [nomino] na kirai [kirai nomino] pia. Sentensi hii inaweza kuwakilishwa kwa kutumia mchoroti kama inavyooneshwa hapa chini;




Hivyo, vipashio vinavyoshirikiana katika kuunda vipashio vikubwa zaidi ndivyo tunavyovichukulia kuwa ni viambajengo. Viambajengo vinavyounda vipashio vilivyo katika hadhi na ngazi tofauti vinaweza kuwa na hadhi sawa kimuundo.

#### 4.2.1.1 Kishazi

Ingawa kishazi hakidhihiriki katika nadharia za kimuundo hasa ile ya Sarufi Miundo Virai [Chomsky, 1957] au Sarufi Geuza Maumbo Zalishi [Chomsky, 1965], kipashio hiki ni muhimu sana katika kujenga sentensi. Mwanaisimu anapochambua sentensi hukizingatia kipashio hiki kama kijenzi cha lazima cha sentensi. Tungo haiwezi kuitwa sentensi pasipo kuundwa na kishazi. Uainishaji wa sentensi hufanywa kwa kuzingatia idadi na aina ya vishazi vinavyoijenga sentensi hiyo. Lyons (1968) katika Massamba na wenzie (1999) ameifasili dhana ya kishazi kama kundi la maneno lenye kiima na kiarifu, hasa likiwa ndani ya sentensi kuu. Kishazi ni kipashio cha kimuundo chenye neno moja au zaidi, kikubwa kuliko kirai na kidogo kuliko sentensi, chenye kitenzi ndani yake na kinachodhihirika ndani ya sentensi. Msingi wa kishazi ni kuwepo kwa kitenzi ndani yake. Mfano;

(a) Baba *amenunua kitanda kikubwa*

(b) Mtoto *alikula matunda* ***yaliyooza***

(c) *Tungefahamiana mapema*, ***tungeishi vyema***

(d) *Ikiwa nitapata fursa*, ***nitashiriki kwenye kongamano***

Sentensi za (a) hadi (d) hapo juu zimeundwa na vishazi. Maneno yaliyopigiwa msitari ndiyo msingi wa kishazi. Maneno haya yanaingia katika kategoria ya kitenzi. Sentensi inaweza kuwa na kishazi kimoja au zaidi. Uamilifu wa kishazi katika sentensi ni kutoa taarifa za mtenda au mtendwa. Viko vishazi vinavyotoa taarifa inayojitosheleza [vishazi viambatani (vishazi huru)]. Vishazi vingine ambavyo havitoi taarifa iliyo kamili huitwa vishazi tegemezi.

Kishazi kiambatani kama kilivyofasiliwa na Massamba na wenzie (1999) ni kishazi ambacho kimeunganishwa katika sentensi kuu na kiunganishi, hasa kiunganishi ‘na’ na ‘lakini’. Kishazi hiki kina sifa kwamba kikiondolewa katika sentensi kuu husimama chenyewe kama sentensi inayojitegemea. Mfano;

(a) Mwalimu wetu anafundisha vizuri ingawa wanafunzi wengi hawampendi

(b) Shule yetu itafungwa kesho lakini mkuu wa shule atabaki shuleni

(c) Tumekuelewa na tutatekeleza

(d) Hata tungemaliza kikao mapema, nisingesafiri*.

Kila tungo hapo juu ina vishazi viwili. Tungo ya (a) mpaka (c) vishazi vyake ni huru kwa sababu hata vikiondolewa katika sentensi hizo na kuwekwa kipekee pekee bado maana ya tungo inapatikana. Vipashio hivyo vitakapoondolewa kwenye sentensi kuu husimama na kuunda sentensi sahili. Ama tungo ya (d) imeundwa kwa vishazi viwili ambavyo kila kimoja kikiondolewa katika sentensi kuu hakiwezi kusimama pekee na kukamilisha maana na/au kuunda sentensi inayojitegemea.

Kishazi tegemezi ni kishazi ambacho hakiwezi kusimama pekee kama sentensi pindi kikiondolewa katika muktadha wa sentensi kuu. Utegemezi huu hutokana na kuwepo kwa **viunganishi tegemezi** kwenye tungo inayohusika, **viambishi vya masharti** na **viambishi virejeshi**. Mfano;

(a) *Japokuwa simpendi*, sitaacha kumsifu

(b) *Ikiwa atatoa ahadi zinazotekelezeka*, nitampa kura yangu

(c) *Asingesoma kwa bidii, asingefaulu mitihani yake*

(d) *Wanafunzi waliofanya vibaya mitihani ya mwisho* wamerudia mwaka

Sentensi za (a) – (d) hapo juu zimeundwa na vishazi viwili kila moja. Vipashio vilivyoandikwa kwa hati za mlalo ni vishazi tegemezi. Vishazi hivi vikiondolewa katika sentensi za hapo juu haviwezi kusimama pekee na kuleta maana iliyokamili. Hivyo, vinaitwa vishazi tegemezi kwa kuwa maana ya sentensi zinazoundwa na vishazi hivi haipatikani pasipo na kuhusisha vishazi vingine (huru).

**Miundo ya Vishazi**

Tumeeleza hapo juu kuwa vishazi vimegawanywa katika vishazi huru na vishazi tegemezi. Vishazi vina miundo yake kama tulivyoieleza hapa chini.

**Miundo ya Vishazi Tegemezi**

i) Vishazi tegemezi vyenye miundo iliyokitwa katika viambishi

Vishazi hivi tegemezi hudhihirishwa kwa kuwepo kwa viambishi rejeshi au viambishi vya masharti ndani ya muundo wake. Miundo ya vishazi hivi imekitwa katika viambishi ***po, ki, ngali na ye***. Mfano:

a) Ali***po***ondoka tulihuzunika.

b) ***Angali***gombania ubunge ***angali***shinda.

c) ***Aki***chelewa kulala atachelewa kuamka.

d) Ali***ye***kua mume wangu amefariki.

ii) Viambishi vitegemezi vyenye miundo iliyokitwa katika neno au maneno.

Katika viambishi tengemezi hivi msingi wake mkubwa ni neno kama vile: ***kama***, ***ili***, ***kwasababu***, na ***japokuwa.*** Mfano;

a) ***Kama*** utakuja kesho, nitakupa zawadi.

b) ***Ili*** ufaulu mtihani lazima usome.

c) ***Kwasababu*** amechelewa ataadhibiwa.

d) ***Japokuwa*** hakufaulu vizuri ataendelea kusoma.

#### 4.2.1.2 Kirai

Kirai ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini hakina muundo wa kiima-kiarifu (TUKI, 1990). Muundo wa kiima-kiarifu ni ule ambao unahusisha mtendaji wa tendo na tendo linalotendwa na ambao ndiyo muundo wa msingi wa sentensi katika lugha yoyote ile iwayo. Kwa maana nyingine tunaweza kusema kuwa tungo kirai ni tungo ya maneno mawili na zaidi ambayo huwa na muundo wa neno kuu linalofuatiwa na maneno mengine kwa mpangilio maalumu unaozingatia uhusiano wa maana ya tungo hiyo. Muundo wa kirai unahusisha neno kuu ambalo aghlabu huwa ndilo jina la kirai husika pamoja na kijalizo au vijalizo. Kijalizo (cha kirai) ni maneno yanayokamilisha taarifa za kirai.

**Aina za Virai:** Miundo ya virai hujikita katika aina za maneno ambazo ndizo chimbuko la mahusiano maalumu ndani ya vipashio hivyo. Hivyo basi tunaweza

kuainisha virai kwa msingi wa aina hizo za maneno ambapo ingawa tunazo aina saba[1] za maneno tunaweza kupata aina tano tu za virai kwa kuwa maneno yenye kufanya kazi za aina moja yamewekwa katika kundi moja la kirai; yaani viwakilishi na nomino vimewekwa kwenye kirai nomino, kielezi na kihisishi vimewekwa katika kirai elezi, na kihusishi na kiunganishi vimewekwa katika Kirai Kihusishi. Aina za virai zinaainishwa hapa chini;

**Kirai Nomino:** Kwa mujibu wa Massamba (2009), kirai nomino ni kirai ambacho muundo wake umekitwa kwenye nomino au mahusiano ya nomino na neno au mafungu ya maneno yanayoambatana nayo. Viwakilishi pia huainishwa kama virai nomino kwa kuwa havitokei pamoja na nomino bali huchukua nafasi ya nomino. Kirai Nomino kina miundo kadhaa. Mfano;

Kirai Nomino kilichoundwa na nomino au kiwakilishi pekee. Mfano;

a) *Maji* yamenywewa

b) *Mtoto* amesafirishwa

c) *Yeye* atarudi kesho

Miundo mingine ya Kirai Nomino ni ile inayohusisha nomino mbili (au zaidi). Mfano;

a) *Mwalimu Hamadi* atasafiri kesho

b) *Baba watoto* ameenda kazini

c) Mwana siasa amefika

[1] Mjadala kuhusu aina za maneno haukupewa nafasi katika kazi hii. Wapo wataalamu waliotaja aina saba za maneno; wengine wametaja aina nane; wengine tisa; n.k. Katika kazi hii tumetumia aina saba za maneno.

Miundo mingine ya Kirai Nomino inahusisha nomino na kivumishi[2] kimoja au zaidi. Mfano:

a) *Mwimbaji mashuhuri* ameumbuka.

b) *Mwamafunzi hodari* amefaulu mitihani yake vizuri.

c) *Madarasa yale matatu makubwa* yatatumika.

Pia Kirai Nomino kinaweza kuundwa na Nomino na Kirai Kihusishi na/au Sentensi kama katika sentensi hizi hapa chini;

a) *Msichana aliyeletwa nyumbani jana* ametoroka.

b) *Jezi walizonunuliwa wachezaji juzi* zimechanika.

c) *Majibu yaliyotafutwa* yamepatikana.

d) *Mtu mwenye miraba mine* ameanguka

e) *Umoja wa vyama vya upinzani* umetetereka

**Kirai Kitenzi**: Hiki ni kirai ambacho kimekitwa katika kitenzi au katika mahusiano ya kitenzi na neno au mafungu ya maneno (Massamba na wenzie, 1999). Kwa maana nyingine unaweza kusema kuwa neno kuu katika kikundi hiki ni kitenzi. Miundo ya virai vitenzi ni ya aina nyingi na ndiyo kiini cha sentensi katika lugha ya Kiswahili na/au lugha nyingine yoyote ile iwayo. Ikumbukwe kuwa miundo ya Kirai kitenzi ni mingi. Hivyo, hapa chini tumetaja miundo michache mno. Kirai kitenzi hutokea kama sehemu muhimu na ya lazima katika sentensi za Kiswahili. Jambo la kuzingatia hapa ni

[2] Maneno mengine yanayohusika kwenye miundo hii tumeyachukulia kama **Vibainishi**. Tutatoa maelezo ya kina kuhusu maneno haya wakati tutakapozungumzia Kirai Bainishi hapo mbele.

uhusiano wa kitenzi na vipashio vinavyokifuata kitenzi hicho. Napo tunaweza kupata miundo ya Kirai kitenzi yenye;

i) Kitenzi Kikuu pekee. Mfano;

a) Ameumia

b) Tutafanikiwa

c) Tutashinda

ii) Kitenzi Kikuu na Nomino (Kirai Nomino). Mfano;

a) Amempa Talaka

b) Ametuma mahari

c) Tumeimbiwa wimbo

iii) Kitenzi Kikuu na Nomino mbili (Kirai Nomino). Mfano;

a) Amemwimbia mtoto wimbo.

b) Amemnunulia Mama Zawadi

c) Amemchapa mwanafunzi viboko

iv) Kitenzi Kisaidizi (Vitenzi Visaidizi) na Kitenzi Kikuu. Mfano;

a) Anapenda kuimba

b) Atakwenda Kusali

c) Alikuwa anataka kuondoka

v) Kitenzi Kishirikishi na Kirai Nomino. Mfano;

a) Juma *ni mtoto wangu*

b) Messi *ndiye mchezaji bora wa dunia*

c) Yeye *si mwalimu mzuri*

vi) Kitenzi Kishirikishi na Kirai Kivumishi. Mfano;

a) Huyo *si mdogo wako*

b) Mtoto wake *ni mpole mno*

c) Kaka yake *ni mtanashati*

vii) Kitenzi Kishirikishi na Kirai Kielezi. Mfano;


a) Kitabu *kipo mezani*

b) Baba *yuko msikitini*

c) Mama hayumo ndani ya nyumba yenu

Katika sarufi miundo virai kwa upande mwingine njia ya matawi ilibuniwa kwa lengo la kuonesha jinsi vipashio (vya Kirai Kitenzi kwa hapa) vinavyomilikiana. Katika kuonesha mahusiano hayo njia ya matawi imekua kama tafsiri ya mshikamano katika kanuni mahususi za lugha, kwa mfano:


S → KN +KT





Njia ya matawi katika mfano hapo juu inaeleza kwamba kipashio kikuu S (Sentensi) kinamiliki vipashio vidogo, Kirai Nomino (KN) na Kirai Kitenzi (KT), kwa mfano;

*Mwalimu anafundisha.*

Sentensi hii inaweza kuchanganuliwa kwa njia ya matawi kama ifuatavyo:




Wanafunzi wamefaulu mtihani vizuri




Hapa tunaona jinsi uhusiano unavyojitokeza. Kila kifundo kinajitokeza moja kwa moja na ama kifundo kingine kinachomilikiwa nacho au na neno linalomilikiwa nalo. Katika miundo hii mahusiano baina ya vitenzi na vipashio vinavyoandamana navyo ni lazima. Hii ina maana kwamba kitenzi kinachohusika kwa maumbile yake ni lazima kiandamane na kipashio au vipashio vya aina yoyote vinavyojitokeza mbele yake. Kwa mfano, kinapo tajwa kitenzi <u>lima</u> msikilizaji anatarajia kitatajwa kinacholimwa. Hii inamaana kila muundo hukitwa kwenye kundi maalumu la kitenzi.

**Kirai Kielezi**: Kirai Kielezi huundwa na kielezi kimoja au zaidi. Tofauti na aina zingine za virai ni kuwa Kirai Kielezi hakielekei kukitwa kwenye mahusiano ya lazima baina ya neno kuu na neno au fungu la maneno linaloandamana nalo na badala yake miundo inayohusika hapa ni ya maneno ambayo hufanya kazi pamoja katika lugha kama misemo, neno au maneno yanayofuata maneno yaliyotangulia yakilifafanua zaidi neno hilo. Maana yetu hapa ni kuwa Kirai Kielezi aghlabu hutokea ndani ya sentensi kama muundo unaojitegemea na usiohusisha maneno mengine zaidi ya maneno yanayofanya kazi pamoja nayo. Kawaida ya Kirai Kielezi ni kutokea kama kijalizo cha Kirai Kitenzi kwamba taarifa zake (Kirai Kielezi) zinafungamana zaidi na kitenzi ingawa mara nyingine hujitokeza kwenye Kirai Kivumishi kama sehemu ya Kirai Nomino. Hivyo, miundo ya Kirai Kielezi si halisi pia ikizingatiwa kuwa vielezi vina uhuru wa kuhama hama katika sentensi. Ipo miundo inayohusisha vielezi pekee, pia ipo miundo inayohusisha vielezi na Virai Husishi. Hapa chini tutataja mifano michache ya sentensi zenye Virai Vielezi (Tumetumia hati za mlalo kuonesha miundo ya Kirai Kielezi). Mfano;

a) Tulifika *juzi mchana*

b) Niletee *mara nyingine*

c) Umemuonea *vibaya sana*

d) Juma anaandika *vizuri*

e) Mama yake anaishi *Jijini Dar es Salaam*

f) Mtoto amekula chakula kidogo *sana*

g) Chumba chake kina mwanga hafifu *mno*

h) Tutaelewana *mbele ya safari*

i) Panya amejificha *chini ya kabati*

j) Mtoto amelala *chumbani mwa mama yake*

**Kirai Kivumishi**: Hiki ni kirai ambacho muundo wake umekitwa katika kivumishi. Kwa kawaida muundo wa kirai hiki huwa na kivumishi na neno au mafungu ya maneno yanayoambatana nayo. Kirai Kivumishi aghlabu huwa kiambajengo cha Kirai Nomino kwa kuwa uamilifu wa kivumishi hutokana na uwepo wa nomino. Maneno aina ya kivumishi ambayo ndiyo yaundayo Kirai Kivumishi huchukua upatanisho wa nomino inayotumika katika sentensi hiyo. Hata hivyo, katika tungo zenye vitenzi vishirikishi, Kirai Kivumishi huainishwa nje ya Kirai Nomino na kwamba huwa muundo unaojitegemea. Miundo ya Kirai Kivumishi ni mingi. Mifano ifuatayo inawakilisha baadhi ya miundo hiyo;

i) Kivumishi na kielezi pekee. Mfano;

a) Amepika chakula *kibaya sana*

b) Amenunua mapambo *mazuri kabisa*

c) Nikatie kitambaa *cheupe pee*

ii) Kivumishi au vivumishi pekee. Mfano;

a) Matunda *mabichi* yamechumwa.

b) Baba amenunua kitanda *kikubwa*

c) Kitambaa *kidogo cheupe* hakionekani

iii) Kivumishi na kielezi nje ya Kirai Nomino. Mfano;

a) Mwalimu wetu ni *hodari sana*

b) Nguo yake ni *ndogo mno*

c) Maneno haya si *mepesi sana*

iv) Kivumishi na Kirai Kihusishi (Kirai Kiunganishi[3]) nje ya Kirai Nomino. Mfano;

a) Chakula hiki ni *kizuri na kitamu*

b) Nyumba yetu ni *mpya yenye rangi ya kuvutia*

c) Wewe ni *hodari wa kuanzisha ugomvi*

**Kirai Kihusishi**: Kirai hiki huundwa na kihusishi pamoja na Kirai Nomino. Aidha, miundo yenye kiunganishi pia baadhi ya wataalamu huibainisha kama Kirai Kihusishi. Hii ni miundo ambayo imekitwa katika mahusiano baina ya maneno *kwa*, *na*, lakini, *katika*, *ingawa*, *ya*, *la*, *cha*, *japokuwa,* au kwenye fungu la maneno linaloandamana nalo. Hivyo basi tunaweza kusema kuwa kirai hiki ni kile ambacho neno kuu ni kihusishi au kiunganishi. Ama miundo yenye kiunganishi, ambayo baadhi ya wataalamu katika Kiswahili wameiainisha kama Kirai Kiunganishi kuna muundo mmoja tu. Huu ni ule muundo wa kiunganishi kufuatwa na kikundi nomino. Muundo huu hautofautiani na miundo mingine ya Kirai Kihusishi. Hivyo, miundo ambayo neno kuu ni kihusishi na/au kiunganishi tumeibainisha kama Kirai Kihusishi. Miundo ya Kirai Kihusishi ipo mingi. Hapa chini tumetaja miundo ifuatayo;

i) Kihusishi na Kirai Nomino. Mfano;

[3] Kirai Kiunganishi tumekieleza kama muundo sawa na Kirai Kihusishi. Hivyo, miundo ambayo neno kuu ni kihusishi au kiunganishi tumeiita kwa jina moja tu la Kirai Husishi.

a) Mtoto *wa baba mdogo* amesafiri

b) Baba *mwenye nyumba* hatafika.

c) Mwanafunzi mtoro ameadhibiwa *na mwalimu wake*

ii) Kihusishi na Kirai Kielezi. Mfano;

a) Niletee saa *ya ukutani*

b) Amelala chumba *cha kati*

c) Gari yake imevunjika kioo *cha mbele*

iii) Kihusishi na Kirai Kitenzi. Mfano;

a) Niletee maji *ya kunywa*

b) Omba dua kabla *ya kulala*

c) Tunafanya mitihani *ya kumalizia muhula*

**Kirai Kibainishi**: Aina hii ya kirai huhusisha maneno aina ya vivumishi kama neno kuu. Maneno haya huelezwa kama vibainishi ingawa kikategoria yanaainishwa kama vivumishi. Yameitwa vibainishi kwa sababu hayataji sifa ya nomino wala kiwakilishi. Kazi yake ni kupambanua na kubainisha nomino, kiwakilishi na/au kivumishi. Hivyo, kama ilivyo kwa Kirai Kivumishi, muundo wa kirai hiki umekitwa kwenye Kirai Nomino. Kirai Kibainishi kina miundo kadhaa inayolingana sana na miundo ya Kirai Kivumishi. Hapa tumetaja mifano michache yenye kuhusisha maneno tuliyoyaita kibainshi. Mfano;

a) Mwanafunzi *wangu* amefika

b) Mtihani *huu* si mgumu sana

c) Kazi *yako hiyo* ina faida tele

Kirai huchukuliwa kuwa kijenzi cha juu katika uchanganuzi wa sentensi. Nadharia ya Sarufi Miundo Virai [SMV] huieleza sentensi kama mkusanyiko wa virai mbalimbali. Uchanganuzi wa sentensi kwa mwongozo wa nadharia hii hulenga kubainisha vijenzi vya sentensi kwa kuanza na virai. Muundo wa sentensi huwakilishwa kwa kutumia kanuni miundo virai [kanuni zalishi], visanduku, au kwa mti wa matawi. Hapa chini tumetoa mfano wa sentensi inayodhihirisha kanuni miundo virai;

*Mtoto mdogo amekula chakula chote kwa kijiko*

1. S -----------→ KN KT
2. KN ---------→ N V
3. KT ---------→ T KN KH
4. KH ---------→ H KN
5. T -----------→ amekula
6. N -----------→ mtoto, chakula, kijiko
7. V -----------→ dogo, chote
8. H ----------- → kwa

(Chanzo: Mdee, 2013)

#### 4.2.1.3 Neno

Neno ni kipashio cha kiisimu ambacho huundwa na mofimu moja au zaidi. Ni mpangilio wa vitamkwa au silabi zenye kutoa umbo lenye maana katika lugha husika.

Ni kijenzi au kipashio kidogo cha kisarufi kinachotoa maana katika lugha inayohusika. Mfano;

a) Anasomesha

b) Mtoto

c) Kitabu *kipya*

**Aina za Maneno**: Upo ukinzani mkubwa baina ya wataalamu wa lugha juu ya uainishaji wa aina za maneno katika lugha mbalimbali. Vigezo vikubwa vinavyotumika katika kuainisha maneno ni kigezo cha kisemantiki, kigezo cha kimofolojia na kigezo cha kisintaksia (Mgullu, 1999). Wako pia wanaotumia kigezo cha kifonolojia katika kuthibitisha kuwa maneno yanaingia katika kategoria anuai. Hata hivyo, katika lugha ya Kiswahili, tofauti kuhusu aina za maneno imejitokeza katika istilahi zilizotumiwa na wataalamu hao pamoja na idadi ya aina za maneno. Mfano, Kihore (1996), Waihiga (1999) na Mgullu (1999) wana aina nane za maneno wakati Kapinga (1983) na Nkwera (1978) wameainisha aina saba za maneno. Wapo waliotaja aina tisa akiwemo Habwe na Karanja (2004) na Khamis (2011).

Mjadala kuhusu idadi na istilahi hatukuupa nguvu katika kazi hii. Pia, makundi ya kila aina ya neno hatukuyazingatia. Jicho letu limejiegemeza zaidi katika mofolojia ya baadhi ya aina za maneno. Hapa tumetumia aina saba zifuatazo za maneno: Nomino, kivumishi, kitenzi, kiwakilishi, kielezi, kihusishi (kiunganishi) na kihisishi. Maneno tuliyoyatumia kwa kina katika mijadala yetu ni nomino na kitenzi. Hata hivyo, kivumishi, kihusishi na kiwakilishi tutakuwa tukiyachambua kila haja ya kufanya hivyo

inapolazimu. Tumechagua aina hizi za maneno (nomino na kitenzi) kwa sababu ndivyo vijenzi vya lazima vya sentensi (pia yanapatikana katika lugha zote), miundo na mjengeko wake ni dhahiri.

**Nomino** ni maneno yanayotaja mtu, kitu, hali au mahali. Katika kila sentensi kunatakiwa kuwa na nomino au kiwakilishi chake. Nafasi ya nomino katika sentensi ni mwanzo (kiima) au baada ya kitenzi (shamirisho). Pia nomino hutokea ndani ya Kirai Kihusishi. Nomino ndiyo hutawala na kupatanisha sarufi ya maneno yote yajengayo sentensi husika. Nomino zina sifa ya kuonesha idadi na ngeli. Muundo wa nomino huhusisha kiambishi awali kinachoonesha idadi na/au ngeli na mzizi wa nomino. Mfano;

| **Umoja** | **Wingi** | **Ngeli** |
|---|---|---|
| a) **M***toto* | **Wa***toto* | M/Wa |
| b) **Ki**tabu | **Vi**tabu | Ki/Vi |
| c) **N**yumba | **N**yumba | N/N |
| d) Jani | **Ma**jani | Ø/Ma |
| e) **M**kono | **Mi**kono | M/Mi |
| f) **U**limi | **N**dimi | U/N |
| g) **U**gonjwa | **Ma**gonjwa | U/Ma |
| h) **U**kuta | Kuta | U/Ø |
| i) **Ku**imba | **Ku**imba | Ku |

**Kitenzi** ni maneno yanayoarifu jambo linalofanywa au kufanyiwa nomino au kiwakilishi chake. Maneno haya yanahusu kutendeka kwa jambo. Kitenzi ndiyo msingi wa utoaji wa taarifa katika sentensi. Vitenzi vinaweza kuelezwa katika sura mbili kuu: vitenzi vinavyohusu utendekaji wa jambo (Vitenzi Halisi) na vitenzi vishirikishi. Vitenzi Halisi ni vitenzi ambavyo huarifu jambo ambalo hufanya au kufanyiwa nomino. Utokeaji wa Vitenzi halisi huweza kuwa kabla au baada ya Nomino. Pia huweza kutokea katika mfululizo wa vitenzi sambamba. Iwapo kitenzi halisi kitatokea katika mpangilio huu, kitenzi kimoja kitakuwa kitenzi kikuu (T) ambacho hubeba hali na maana kuu ya tendo, na kitenzi kingine kitakuwa kitenzi kisaidizi (Ts). Kitenzi halisi hubeba mofu ya njeo, nafsi, masharti, urejeshi, kauli, hali, dhamira na mzizi wa kitenzi. Ama vitenzi vishirikishi, hivi ni vitenzi ambavyo hushirikisha hali mbalimbali kihali, kimazingira na kitabia. Mfano;

a) Mtoto *analia*

b) Maida *alikuwa anataka kusafiri*.

c) Wazalendo *wanatakiwa kupigania* nchi yao.

d) Huyu *si* mjinga

e) Mimi *ndiye* mshindi

f) Mwembe wetu *ni* mrefu

### 4.2.2 Miundo ya Sentensi za Kiswahili Sanifu (KS)

Wataalamu wa sintaksia wameeleza miundo mitatu ya sentensi: sentensi sahili, sentensi changamani na sentensi ambatani. Massamba na wenzake (2009) na Matinde (2012) wanasema kuwa Sentensi Sahili ni Sentensi ambayo imeundwa na Kirai Nomino na

Kirai Kitenzi ambayo huleta maana kamili iliyokusudiwa. Pia, wameifasili Sentensi Changamano kuwa ni Sentensi ambayo huundwa na vishazi huru pamoja na vishazi tegemezi vyenye miundo iliyokitwa kwenye viunganishi tegemezi, viambishi vya masharti na viambishi rejeshi ndani yake kama vile (amba-) au (-o-) au (-ye-) au (-nge-) au (ikiwa). Massamba na Matinde (weshatajwa) wanaifasili Sentensi Ambatano kuwa ni Sentensi ambayo imeundwa na vishazi huru viwili au zaidi, vishazi hivyo huunganishwa na viunganishi kama vile lakini, ingawa, tena, ila, wala, n.k.

Sentensi za lugha yoyote ile hujengwa na vipashio maalumu. Vipashio vya lugha ni vipengele ambavyo kwa pamoja huijenga lugha hiyo. Sentensi ndicho kipashio kikubwa cha lugha. Vipashio vya lugha viko katika viwango vitano ambavyo ni mofu, neno, kirai, kishazi na Sentensi. Kila kipashio huwa na uamilifu na/au maana fulani. Vipashio vya lugha hupishana na kutofautiana kihadhi, baadhi ni vidogo na vingine ni vikubwa. Kwa kawaida vipashio hivyo huwa vina sifa ya kujengana yaani vidogo huungana na kujenga vipashio vikubwa zaidi. Mshikamano wa vipashio hufanywa kwa utaratibu maalumu kuanzia kipashio cha chini [mofu] hadi kipashio cha juu kabisa [Sentensi] (Matinde, 2012; Massamba na wenzake, 1999).

Kwa mujibu wa nadharia ya Sarufi Miundo Virai uchanganuzi wa sentensi huhusu ubainishaji wa vinavyojenga sentensi. Viambajengo vikuu ni virai ambavyo huundwa na maneno. Maneno na virai kama vilivyoelezwa katika nadharia hii hujengwa na vipashio vingine anuai. Ndipo wanasarufi Msonge (Halliday, 1961; Berry, 1977) waliposema kuwa sentensi ndicho kipashio kikubwa kuliko vipashio vingine katika

lugha. Sentensi huundwa na kishazi kimoja [huru] au zaidi; kishazi huundwa na kirai kimoja au zaidi; kirai huundwa na neno moja au zaidi; na neno huundwa na mofu moja au zaidi. Kwa mfano:

(i) Mofu kuunda neno. Mfano;

(a) m+tu (Mofu mbili)

(b) a+li+andik+a (mofu nne)

(ii) Maneno kuunda kirai. Mfano;

(a) Kitabu + changu (maneno mawili)

(b) Chini + ya + mti + mkavu (maneno manne)

(iii) Virai kuunda kishazi. Mfano;

(a) Muhula mpya + wa masomo + utaanza + wiki ijayo (virai vinne)

(b) Mitihani + tuliyofanya + mwaka jana + imefutwa (virai vinne)

(iv) Vishazi kuunda Sentensi. Mfano;

(a) Ikiwa tutajitahidi katika masomo + tutapata matokeo mazuri (vishazi viwili)

(b) Chai iliyopikwa asubuhi + imenywewa yote (vishazi viwili)

Lengo la lugha siku zote ni kufanikisha mawasiliano. Kipashio cha uzungumzaji na kinachojitosheleza katika mawasiliano ni sentensi. Ili mawasiliano fanisi yapatikane ni muhimu kuzungumza kwa kutumia Sentensi zinazoeleweka kwa walengwa. Sentensi hizo lazima ziwe na mpangilio mzuri wa maneno na miundo mingine inayojenga

sentensi zinazokubalika katika jamii husika. Kinyume na hayo, mawasiliano fanisi hayapatikani. Sentensi za Kiswahili zina miundo maalumu. Miundo hiyo inabainika katika mitindo ya lugha inayotumika katika mawasiliano yafanywayo kwenye mazingira anuai. Katika sehemu hii tulijadili miundo ya sentensi itumiwayo katika Kiswahili sanifu kwenye lengo la kwanza na miundo ya sentensi itumiwayo katika Kiswahili cha lahaja ya Kipemba [tu] katika lengo la pili. Tulijadili vijenzi vya sentensi kwa ujumla wake kisha tulijikita na vipashio (vishazi) mahususi vijengavyo kila aina ya sentensi.(marekebisho)

#### 4.2.2.1 Sentensi Zenye Miundo Sahili

Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (2009) na Matinde (2012), Sentensi Sahili ni Sentensi ambayo imeundwa na Kirai Nomino na Kirai Kitenzi ambayo huleta maana kamili iliyokusudiwa. Muundo huu huelezwa dhahiri kwa kutumia nadharia ya Sarufi Miundo Virai. Aina hii ya sentensi hujengwa na kishazi kimoja tu. Kawaida ya kishazi hiki ni kuwa huru. Kishazi hiki lazima kiweze kusimama pekee na kujitosheleza katika kuchanuza maana ya tungo. Sifa ya kishazi huru ni kwamba hata kinapoondolewa katika muktadha wa sentensi kuu basi huweza kusimama pekee kama sentensi. Mfano;

a) Watoto watatu wamepotea

b) Serikali yetu inatuhurumia

c) Muombe Mungu

d) Tunafanya kazi kwa bidii

e) Yeye ni rafiki yangu

f) Baba amenunua kitanda kikubwa

g) Watoto wake wadogo wamenunua matunda matamu

h) Kijana mwenye hasira ameondoka

i) Mwalimu Khamis hajafika

j) Kisu chake kimepotea tangu Ijumaa

k) Mkutano wa waandishi wa habari utafanyika leo jioni

l) Wanachama wa vikundi vya ushirika wameandamana


m) Mwanafunzi wangu ana masihara sana

n) Mkuu wa mkoa atahutubu kesho


o) Matunda tuliyokula leo asubuhi ni matamu mno

Kama tulivyoonesha hapo juu kuwa sentensi hizi huundwa na kishazi huru kimoja tu. Muundo wa sentensi hizi huhusisha Kirai Nomino na Kirai Kitenzi. Miundo hii ya Kirai Nomino na Kirai Kitenzi inaweza kuhusisha miundo mingine anuai kama tulivyoieleza kwenye uchambuzi wa virai. Hapa chini tutatumia mchoroti kuchanganua miundo miwili tu ya sentensi sahili ili kuweka wazi zaidi maelezo yetu.

a) Watoto wake wadogo wamenunua matunda matamu



b) Tunafanya kazi kwa bidii




**4.2.2.2 Sentensi Zenye Miundo Changamani**

Wataalamu kama Massamba na wenzake (2009) na Matinde (2012) wanaifasili Sentensi Changamano kuwa ni Sentensi ambayo huundwa na vishazi huru na vishazi tegemezi. Aina hii ya sentensi inajumuisha vishazi vya aina zote yaani vishazi viambatani na vishazi vitegemezi. Utegemezaji wa vishazi ndio msingi wa uundaji wa sentensi changamani. Utegemezi huu unaweza kutokana na matumizi ya viambishi rejeshi (-ye-, -lo-,-vyo-, -po-, -o-, n.k.) ndani ya umbo la kitenzi au mwishoni mwa mzizi wa neno amba-. Uundaji wa sentensi changamani pia unaweza kutokana na matumizi ya viambishi vya masharti, matumizi ya viunganishi tegemezi na matumizi ya

vijalizo. La muhimu zaidi ni kuwa kishazi tegemezi kinaweza kuwa kimoja au zaidi katika miundo ya sentensi changamani lakini kishazi kiambatani lazima kiwe kimoja tu. Mfano;

a) Wachezaji walipongezwa waliposhinda mfululizo

b) Ikiwa hutajali, nitakuomba msaada

c) Nyumba waliyohama inauzwa

d) Walimu wetu wanatuhurumia tunapopatwa na matatizo darasani

e) Japokuwa sina pesa za nauli, ninalazimika kusafiri

f) Kila unapohisi kukata tamaa, muombe Mungu

g) Ukitaka kufanikiwa katika maisha, fanya kazi kwa bidii

h) Mvua iliyonyesha msimu huu imenawirisha mazao

i) Kitabu ulichoniazima kimenipa faida kubwa

j) Kazi uliyofanya leo imekusumbua sana

k) Wanafunzi watoro huadhibiwa wanapofanya vibaya kwenye masomo yao

l) Hata kama hutanichagua, nitashinda tu

m) Kama umemaliza unaweza kwenda


n) Usifanye masihara katika mambo yanayohitaji umakini

o) Usingenikumbusha nisingekumbuka kamwe.


Tumesema hapo awali kuwa miundo ya Sentensi Changamani hushirikisha vishazi vya aina zote mbili. Tuongezee hapa kuwa kishazi huru kinaweza kuondolewa katika muktadha wa sentensi kuu na bado kikasimama kama sentensi yenye kujitegemea. Ama kishazi tegemezi, kutokana na kuwa kwake tegemezi, pindi kikiondolewa katika

muktadha wa sentensi kuu, hakiwezi kujitegemea. Kishazi hiki (kishazi tegemezi) huwa ni kijenzi (kiambajengo) cha Kirai Nomino au kirai tenzi cha sentensi kuu. Hapa chini tutatumia mchoroti kuchanganua miundo miwili tu ya sentensi changamani ili kuweka wazi zaidi maelezo yetu.

a) Wanafunzi watoro huadhibiwa wanapofanya vibaya kwenye masomo yao




b) Kazi uliyofanya leo imekusumbua sana



#### 4.2.2.3 Sentensi Zenye Miundo Ambatani

Sentensi Ambatano imefasiliwa kuwa ni Sentensi ambayo imeundwa na vishazi huru viwili au zaidi vilivyounganishwa na viunganishi kama vile, lakini, ingawa, tena, ila, wala, n.k. Aina hii ya sentensi huhusisha vishazi viambatani zaidi ya kimoja. Santensi Changamani pia hujitokeza kushirikiana na kishazi kiambatani katika kuunda sentensi ambatano. Jambo la lazima katika sentensi ambatani ni kuwepo kwa uunganishaji wa miundo miwili au zaidi yenye kujitegemea. Aidha, miundo inayounganishwa sharti iwe inachukuana kimaana. Sentensi Ambatani ina miundo mingi. Hapa chini tumetaja mifano ya sentensi ambatani. Mfano;

a) *Tupendane* na *tuhurumiane* ili *tushikamane pamoja*

b) *Hawapendi kusoma* wala *kuandika*

c) *Mama yake ni mwalimu* na *baba yake ni daktari*

d) *Tumejiandaa kusafiri* japokuwa *hatuna hati za kusafiria*

e) *Matokeo yamechelewa kutoka* kwa sababu *walimu wamechelewa kusahihisha*

f) *Mtoto aliyepotea jana ameonekana* na *amerudishwa kwa wazazi wake*

g) *Ungefika mapema ungemkuta* hata kama *asingekusikiliza*

h) *Mtoto wako ni hodari sana* lakini *anapenda kucheza*

i) *Baba yake atasafiri kesho* japokuwa *kazi aliyopewa hajaikamilisha*

j) *Rafiki yake ni mwenyekiti wa mtaa* ingawa *yeye hana kitambulisho*

k) *Jitambulishe* ingawa *wengi wanakufahamu*

l) *Baba yake ni mwalimu wangu* na *mtoto wake ni mwanafunzi wangu*


m) *Haoni* wala *hasikii*

n) *Alifanya kazi kwa bidii* lakini *hakulipwa*


o) *Mtihani huu si mgumu* japokuwa *hatutafaulu sana*

Tumeeleza hapo awali kuwa sentensi ambatani zinahusisha sentensi zaidi ya moja. Ni muundo wa sentensi unaotumiwa kuunda sentensi ndefu na zisizo ukomo. Viunganishi hutumiwa katika kuunda sentensi ambatani ambazo kutokana na urefu wake baadhi yake huitwa sentensi uchamko. Kama tulivyobainisha kuwa miundo ya sentensi ambatani inahusisha sentensi zaidi ya moja, uchanganuzi wake lazima uoneshe kuwa sentensi kuu inaundwa na sentensi mbili au zaidi. Hapa chini tutatumia mchoroti kuchanganua miundo miwili tu ya sentensi ambatani ili kuweka wazi zaidi maelezo yetu.

a) *Tupendane* na *tuhurumiane* ili *tushikamane pamoja*



b) *Mama yake ni mwalimu* na *baba yake ni daktari*




Kwa ujumla, sentensi za Kiswahili zinahusisha miundo mikuu mitatu: sentensi sahili, sentensi changamani na sentensi ambatani. Tumeona namna vishazi viambatani na vishazi vitegemezi vinavyoweza kuunda aina hizo za sentensi. Tumeona namna miundo hiyo ya vishazi inavyoundwa kutokana na virai mbalimbali. Tumeona jinsi virai vinavyoundwa kutokana na aina tofauti za maneno. Tumeona pia jinsi maneno yanavyoundwa kutokana na mfuatano mzuri wa mofu. Sehemu inayofuata tumejadili kwa kina miundo mikuu mitatu ya sentensi za lahaja ya Kipemba: sentensi sahili, sentensi changamani na sentensi ambatani.

### 4.2.3 Miundo ya Sentensi za Lahaja ya Kipemba (KP)

Uchambuzi wa sentensi zilizokusanywa katika maeneo mbali mbali ya lahaja ya Kipemba umezingatia mgawanyo wa sentensi sahili, sentensi changamano na sentensi ambatano. Sentensi hizi zimegawanywa katika makundi hayo matatu [sentensi sahili, sentensi changamano na sentensi ambatano] kwa msingi uleule wa kuangalia kipashio (kiambajengo) kinachojenga sentensi (yaani kishazi). Sentensi yenye kishazi kiambatani kimoja tu tumeiweka katika kundi la sentensi sahili; sentensi yenye kishazi au vishazi tegemezi na kishazi kiambatani kimoja tu tumeiweka katika sentensi changamano; na sentensi yenye vishazi viambatani viwili au zaidi (bila kujali kuwepo au kutokuwepo kwa kishazi au vishazi tegemezi) tumeiweka katika sentensi ambatano.

Tukumbuke kuwa kishazi kimejengwa na vipashio vilivyo chini yake (yaani virai na maneno). Vishazi vinavyounda sentensi za lahaja ya Kipemba vina sifa isiyotofautiana (sana) na vishazi vinavyounda sentensi za Kiswahili sanifu. Lakini, mpangilio na mfuatano wa viambajengo vinavyojenga vipashio hivyo unaweza kutofautiana kwa baadhi ya sentensi zitumiwazo na baadhi ya maeneo ya Wapemba. Jambo hili tumelijadili kwa kina huko mbele wakati tukizungumzia tofauti baina ya sentensi za Kipemba na sentensi za Kiswahili sanifu. Baadhi ya miundo ya Kirai Nomino cha Kipemba, Kirai Kitenzi cha Kipemba, kitenzi cha Kipemba, na vipashio vingine unajipambanua unapohusishwa na vipashio hivyo hivyo katika Kiswahili sanifu. Dhana ya kiangami, uunganishaji, udondoshaji na/au uongezaji, ngeli ya N/Wa ni baadha ya miundo ambajengo katika vipashio vijengavyo sentensi za lahaja ya Kipemba.

#### 4.2.3.1 Sentensi za Kipemba Zenye Miundo Sahili

Kama tulivyoeleza hapo awali kuwa sentensi sahili ni sentensi zenye kishazi kiambatani kimoja tu. Sentensi hizi kimuundo zina sifa ileile ya sentensi za Kiswahili sanifu. Ama muundo wa vipashio viundavyo sentensi za lahaja ya Kipemba unaweza kutofautiana na muundo wa vipashio vya sentensi za Kiswahili sanifu. Tofauti hizo za muundo wa vipashio wa miundo ya sentensi za Kiswahili Sanifu na ule wa sentensi za Kipemba tumezieleza huko mbele. Sentensi sahili za lahaja ya Kipemba kama zilivyo sentensi sahili za Kiswahili sanifu, zina miundo kadhaa. Miongoni mwa miundo hiyo ni;

i) Kirai Kitenzi pekee[4]. Mfano;

a) Kashaanka (KP)
Ameamka (KS)

b) Heuka (KP)
Hakuondoka (KS)

c) Achezavye (KP)
Anacheza (KS)

ii) Kirai Kitenzi na Kirai Nomino. Mfano;

a) Kashakula chungwangwa (KP)
Amekula chungwa la watu (KS)

b) Kanchukua bukungwa (KP)
Amechukua daftari la watu (KS)

c) Yuacheza mpira (KP)
Anacheza mpira (KS)

[4] Tazama sifa za sentensi za Kiswahili kama zilivyobainishwa na Massamba na wenzie (1999).

iii) Kirai Kitenzi na Kirai Elezi. Mfano;

a) Kankwenda chuoni (KP)
Ameenda madrasa (KS)

b) Kashakwendavye kwao (KP)
Ameenda nyumbani (KS)

c) Kansimama nlangoni (KP)
Amesimama mlangoni (KS)

iv) Kirai Nomino na Kirai Kitenzi. Mfano;

a) Mvyelewe Mwamboga ka’nkugwa (KP)
Mzazi wake Mwanamboga ameanguka (KS)

b) Asya nmwanangu (KP)
Asia ni mtoto wangu (KS)

c) Ng’ombengwa za kake zin’geleka tokea majuzi (KP)
Ng’ombe wa kaka wamepotea tangu juzi (KS)

d) Nekwenda uko bandani kuzinga kitooyo (KP)
Nilienda kutafuta kitoweo huko kwenye soko (KS)


e) Nkateo unkugwashi (KP)
Mkate wako umeanguka chini (KS)

f) Mameye yu ndanimwe (KP)
Mama yake yumo ndani mwake (KS)


g) Wanangu wadigi hawebu hogo chungu (KP)
Watoto wangu wadogo hawataki muhogo mchungu (KS)

Hapa chini tumetumia mchoroti kuchanganua miundo miwili tu ya sentensi sahili za lahaja ya Kipemba ili kuweka wazi zaidi maelezo yetu.

a) Wanangu wadigi hawebu hogo chungu




b) Ng’ombengwa za kake zin’geleka tokea majuzi




**4.2.3.2 Sentensi za Kipemba Zenye Miundo Changamani**

Tumeeleza hapo awali, wakati tulipozungumzia sentensi za Kiswahili sanifu kuwa sentensi changamani hujengwa na kishazi tegemezi au vishazi tegemezi pamoja na kishazi ambatani kimoja tu. Tumeeleza kuhusu sababu za utegemezi wa kishazi tegemezi kwamba husababishwa na maneno (viunganishi) tegemezi, viambishi rejeshi, viambishi vya masharti, n.k. Vivyo hivyo kwa sentensi changamani za lahaja ya Kipemba kwamba muundo wake unahusisha kwa pamoja vishazi vya aina zote mbili;

yaani vishazi tegemezi pamoja na vishazi ambatani. Isipokuwa, miundo ya vipashio vinavyojenga vishazi hivyo unaweza kuwa tofauti kwani lahaja ya Kipemba inajipambanua (sana) ilinganishwapo na Kiswahili sanifu. Sehemu hii tumebainisha mifano kadhaa ya sentensi changamani za lahaja ya Kipemba. Tunachoweza kusisitiza hapa ni kuwa, uchangamani wa sentensi hizi pia unatokana na kuwepo kwa kishazi au vishazi tegemezi pamoja na kishazi ambatani. Mfano;

a) Mvyelewe Mwamize alipopata ajali ekufa papo apo (KP)
Mzazi wake Mwanamize alipopatwa na ajali alikufa hapo hapo (KS)

b) Walipoegesha pekuwa na mbuyu (KP)
Walipoegesha palikuwa pana m'buyu (KS)

c) Alipokufa bibiye miye seepo (KP)
Bibi yake alipokufa mimi sikuwepo (KS)

d) Ntoto aliyegeleka heonekwa (KP)
Mtoto aliyepotea hakuonekana (KS)

e) Alipovyaa hetaka kwenda sipitali (KP)
Alipozaa hakutaka kwenda hospitali (KS)

f) Ng'ombeyo iliyokata kamba inaonekwa kisimani yanywa maji (KP)
Ng'ombe wako aliyekata kamba ameonekana anakunywa maji kisimani (KS)

g) Mwanao hwemuona alivonipigia mwanangu (KP)
Mtoto wako hukumuona alivyompiga mtoto wangu (KS)

h) N'gaiya miye iyo simuyo iliyobovuka kioo (KP)
Nipe mimi simu yako hiyo iliyoharibika kioo (KS)

i) Wengekawia kidigi tu wengekuja nshauka (KP)
Ungechelewa kidogo tu ungekuja nishaondoka (KS)

j) Weye twaa kyokyote utakakyo (KP)
Wewe chukua chochote unachokitaka (KS)

k) Kama watakapata kiti usijekawia nno (KP)
Ikiwa unataka kupata kiti usichelewe sana (KS)

l) Ule nkate uliobakisha alipokula ntoto nnauchukua miye (KP)
Mkate uliobaki alipokula mtoto nimeuchukua mimi (KS)

m) Kanfise kakeyo duka uliyonunua shunvi (KP)
Ukampeleke kaka yako kwenye duka ulilonunua chumvi (KS)

n) Nnamuona n'duka alivonkimbia asikari (KP)
Nimemuona mwenye duka alivyomkimbia askari (KS)

o) Akiuka mapema hebufuatwa ni ntu (KP)
Akiondoka mapema hatafuatwa na mtu (KS)

Tukichunguza mifano hapo juu tutabaini kuwa sentensi hizo zote ni changamani. Sentensi hizo zimeundwa kwa kishazi au vishazi tegemezi pamoja na kishazi huru. Sentensi hizo zina vipashio vinavyoshusha hadhi ya vipashio vinavyojenga sentensi. Vipashio hivyo ni pamoja na viambishi rejeshi, viunganishi tegemezi pamoja na viambishi vya masharti. Iko miundo mingine inayoweza kuchukuliwa kama sentensi changamani lakini hatukuihusisha katika kazi hii. Sababu za kutoihusisha ni kuwa vishazi vyake vina hadhi sawa kimuundo lakini vinatofautiana kidhima tu. Sentensi hizi ni zile zilizoelezwa na baadhi ya wataalamu kuwa zinaundwa na vitenzi jina. Wataalamu wengine kama Chomi (2001, 2003) ameziita kuwa ni sentensi kunjiano. Kishazi cha kwanza ambacho aghlabu hukaa mwanzoni mwa sentensi hufanya kazi ya kupatanisha maneno mengine yanayounda sentensi husika. Mifano ya sentensi hizi ni;

a) Kulyako shibe uko kutakuavya roho (KP)
Kula kwako huko sana kutakutoa roho (KS)

b) Kuavyakwe mimba kwen'nyima pyaa (KP)
Kutoa kwake mimba kumemkosesha mambo mengi sana (KS)


c) Kugeleka kwa mwanawe kunantia kihoro (KP)
Kupotea kwa mtoto wake kumemtia simanzi (KS)

d) Kuchelewakwe hekwetuharibia (KP)
Kuchelewa kwake hakukutuathiri (KS)


e) Kutembeakwe pekupeku kwenzuru (KP)
Kutembea kwake pekupeku kumemuathiri (KS)

Ukichunguza kwa makini sentensi za hapo juu utaona kuwa ndani ya kila sentensi kuna vitenzi vikuu viwili. Vitenzi hivyo ndivyo vinavyounda vishazi ambatani vya sentensi hizo. Kishazi kilichokaa mwanzo wa sentensi kinasimamia upatanisho wa kisarufi katika sentensi husika. Baadhi ya wataalamu wamezichambua sentensi za aina hii kama zichambuliwavyo sentensi sahili. Hii ndiyo sababu iliyotufanya muundo wa sentensi wa aina hii tusiuhusishe katika mifano yetu ya sentensi changamani. Hapa chini tumetumia mchoroti kuchanganua miundo miwili tu ya sentensi changamani za lahaja ya Kipemba ili kuweka wazi zaidi maelezo yetu.

a) Ng'ombeyo iliyokata kamba inaonekwa kisimani yanywa maji



b) N’gaiya miye iyo simuyo iliyobovuka kioo




**4.2.3.3 Sentensi za Kipemba Zenye Miundo Ambatani**

Sentensi ambatani za lahaja ya Kipemba zina miundo yenye kuhusisha vishazi viambatani viwili au zaidi. Vishazi hivyo huwekwa pamoja kwa kutumia viunganishi. Miundo ya sentensi ambatani za lahaja ya Kipemba pia huhusisha sentensi sahili mbili au zaidi. Wakati mwingine sentensi sahili huungana na sentensi changamani. Ipo miundo ya sentensi ambatani inayohusisha sentensi changamani mbili au zaidi. Uunganishaji huo ndio msingi wa sentensi ambatani. Uunganishaji wa aina hiyo hufanywa kwa kutumia maneno unganishi kama vile kama, kuwa, ela, bali, ta kama, ilhali, japo, japokuwa, ta, na mengineyo. Mfano;

a) Uwo moto uchukule ukautile uko zikoni (KP)
Uchukue moto huo na ukautie huko jikoni (KS)

b) Kazinge nshi tutwange (KP)
Katafute mchi tutwange (KS)

c) Nchukule umpakate unkererishe (KP)
Mchukue, umpakate, umkalishe kitako (KS)

d) Uyo mwana kashapisa, kankitia kuni gimbigimbi (KP)
Mtoto huyo ameunguza chakula, ametia kuni nyingi sana (KS)

e) Fatuma njoo nisongee huyu mwanangu (KP)
Fatuma njoo unisukie huyu mtoto wangu (KS)

f) Nenda jikoni ukagose moto (KP)
Nenda jikoni ukafanye moto (KS)

g) Alipoiba ekamatwa akapigiwa kyannadi (KP)
Alipoiba alikamatwa alinadiwa mwizi (KS)

h) Nekwenda chezea jua, hitaka awa roho (KP)
Nilikwenda kuchezea jua, nilitaka kutokwa na roho (KS)

i) Mtoto kamaiba na shahidi kaapo aketwe (KP)
Mtoto ameiba na shahidi yupo akaitwe (KS)

j) Neumwa sukuli ela hakuna ntu ta: mmoja aliyesema tun'gwiye nkono tukanfise (KP)
Niliumwa shule lakini hakuna mtu hata mmoja aliyesema tukamkamate mkono tumpeleke nyumbani (KS)

k) Dade shika kyombokyo ela kile kikombekyo kin'vunjika (KP)
Dada shika chombo chako lakini kile kikombe chako kimevunjika (KS)


l) Fatuma euka apa nzima ela alipofika nyumbanikwe ebwagwa ni homa (LKP)
Fatuma alipoondoka hapa ni mzima ila aliumwa na homa alipofika nyumbani kwake (KS)

m) Netaka bukule elakini hewahi nipa (LKP)
Nilitaka daftari lake lakini hakuwahi kunipa (KS)


Sentensi ambatani tumezieleza hapo awali kuwa zinahusisha sentensi zaidi ya moja au vishazi ambatani viwili au zaidi. Sentensi hizi zina miundo kadhaa. Mara nyingi mazungumzo hutawaliwa na sentensi za aina hii. Sentensi hizi hujitokeza sana kwenye sentensi uchamko hasa ukizingatia kuwa uunganishaji ndio msingi wa uundaji wa

sentensi hizo (yaani, sentensi ambatani na sentensi uchamko). Hapa chini tumetumia mchoroti kuchanganua miundo miwili tu ya sentensi ambatani za lahaja ya Kipemba ili kuweka wazi zaidi maelezo yetu.

a) Netaka bukule elakini hewahi nipa




b) Dade shika kyombokyo ela kile kikombekyo kin’vunjika



## 4.3 Ulinganishaji wa Miundo ya Sentensi za Kiswahili Sanifu (KS) na Sentensi za Lahaja ya Kipemba (KP) na Namna Zinavyokwamisha Mawasiliano Fanisi

Data zilizopo (4.2 na vipengele vyake) na (4.3 na vipengele vyake) hapo juu zilihusu miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba. Tumeeleza na kuchambua kwa uwazi miundo ya sentensi sahili, sentensi changamani na sentensi ambatani katika pande zote mbili. Tumeona kuwa sentensi za lahaja ya Kipemba na sentensi za Kiswahili sanifu zinaundwa na vishazi. Kishazi ambatani kimoja tu ndicho kinachounda sentensi sahili. Kishazi tegemezi au vishazi tegemezi pamoja na kishazi ambatani kimoja tu ndivyo vijenzi vya sentensi changamani. Vishazi ambatani viwili au zaidi ndivyo vijenzi vya sentensi ambatani. Sehemu inayofuata tumeelezea mfanano baina ya miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba; tofauti baina ya miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba; na athari za kimawasiliano zinazotokana na tofauti baina ya miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba.

### 4.3.1 Uwiano baina ya Miundo ya Sentensi za Kiswahili Sanifu na Miundo ya Sentensi za Lahaja ya Kipemba

Miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba inafanana kwa kiasi kikubwa sana. Ukirejea data za hapo juu utagundua kuwa miundo yenye sentensi sahili, miundo yenye sentensi changamani na miundo yenye sentensi ambatani imedhihirika kote [kwenye Miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu na miundo

ya sentensi za lahaja ya Kipemba]. Sifa za kimuundo baina ya miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba zinafanana.

#### 4.3.1.1 Muundo wa Sentensi Sahili za Lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu

Zote, sentensi sahili za Kiswahili sanifu na sentensi sahili za lahaja ya Kipemba zinaundwa na kishazi ambatani kimoja tu. Ipo miundo kadhaa ya sentensi sahili za Kiswahili sanifu kama ilivyo kwa sentensi sahili za lahaja ya Kipemba. Muundo unaohusisha Kirai Nomino na Kirai Kitenzi [KN + KT] na muundo unaohusisha Kirai Tenzi [KT] pekee ndiyo miundo mikuu ya sentensi sahili za Kiswahili sanifu na sentensi sahili za lahaja ya Kipemba. Zote zinayo miundo mingine kadhaa inayotokana na miundo miwili hii kama tulivyotoa mifano katika kipengele vya hapo juu.

#### 4.3.1.2 Muundo wa Sentensi Changamani za Lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu

Zote, sentensi changamani za Kiswahili sanifu na sentensi changamani za lahaja ya Kipemba zinaundwa na kishazi au vishazi tegemezi pamoja na kishazi ambatani kimoja tu. Ipo miundo kadhaa ya sentensi changamani za Kiswahili sanifu kama ilivyo kwa sentensi changamani za lahaja ya Kipemba. Kishazi tegemezi kinachohusika katika miundo ya sentensi changamani za Kiswahili sanifu na miundo ya sentensi changamani za lahaja ya Kipemba kimehusisha viunganishi tegemezi, viambishi rejeshi au viambishi vya masharti. Vishazi tegemezi vinavyoundwa na viambishi rejeshi vinavyohusika katika miundo ya sentensi changamani za Kiswahili sanifu na sentensi changamani za lahaja ya Kipemba hujitokeza kama viambajengo vya Kirai Nomino au

Kirai Kitenzi. Mifano tuliyoitoa kwenye maelezo yetu kuhusu sentensi changamani za Kiswahili Sanifu na Sentensi Changamani za lahaja ya Kipemba ni kielelezo cha maelezo haya.

#### 4.3.1.3 Sentensi Ambatani Zinaundwa na Vishazi Ambatani Viwili au Zaidi

Zote, sentensi ambatani za Kiswahili Sanifu na sentensi ambatani za lahaja ya Kipemba zinaundwa na vishazi ambatani viwili au zaidi. Ipo miundo kadhaa ya sentensi ambatani za Kiswahili sanifu kama ilivyo kwa sentensi ambatani za lahaja ya Kipemba. Miundo ya sentensi ambatani za Kiswahili Sanifu na miundo ya sentensi ambatani za lahaja ya Kipemba huhusisha viunganishi kama msingi wa uunganishaji wa vishazi viwili au zaidi na/au sentensi mbili au zaidi. Sentensi zinazoweza kuunganishwa hapa huwa sahili na/au changamani. Sentensi ambatani za Kiswahili Sanifu na sentensi ambatani za lahaja ya Kipemba huweza kuwa na sura ya sentensi uchamko pia. Mifano tuliyoitoa kwenye maelezo yetu kuhusu sentensi ambatani za Kiswahili Sanifu na sentensi ambatani za lahaja ya Kipemba ni kielelezo cha maelezo haya.

### 4.3.2 Tofauti Baina ya Miundo ya Sentensi za Kiswahili Sanifu na Miundo ya Sentensi za Lahaja ya Kipemba

Ingawa tumeeleza hapo awali kuwa miundo ya sentensi za Kiswahili Sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba inafanana kwa kiasi kikubwa sana lakini kuna tofauti zinazojitokeza katika vipashio vinavyounda virai. Haidhuru ukirejea data zetu za hapo juu utagundua kuwa miundo yenye sentensi sahili, miundo yenye sentensi changamani na miundo yenye sentensi ambatani imedhihirika kote [kwenye miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba]. Pamoja na kuwa sifa za

kimuundo baina ya miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba zinafanana, kwa kuwa tumeeleza kuwa viambajengo vya sentensi [ambavyo kwa hapa tunakusudia kishazi] vinaundwa na vipashio vilivyo chini yake [yaani, vipashio vidogo kuliko kishazi: virai na maneno], sehemu hii tulieleza tofauti baina ya miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba. Tumeegemeza mjadala wetu kwenye vipashio vinavyojenga vishazi vinavyounda sentensi husika.

#### 4.3.2.1 Kategoria za Kileksika (Maneno)

Kategoria za kileksika ni jumla ya maneno yote yanayotumika katika lugha. Hiki ni kipashio muhimu na cha lazima katika ujenzi wa sentensi. Kategoria za kileksika ndicho kipashio cha chini cha uchanganuzi wa sentensi kwa mujibu wa sarufi mapokeo. Katika sintaksia, ambapo sentensi ndiyo hushughulikiwa, kategoria za kileksika (maneno) na virai ndizo kategoria za msingi. Hivyo, sentensi za Kiswahili sanifu na sentensi za lahaja ya Kipemba zinaundwa na kategoria za kileksika. Isipokuwa, kategoria za kileksika nyingi zinazotumiwa katika ujenzi wa sentensi za lahaja ya Kipemba hazipatikani katika sentensi za Kiswahili sanifu.

Kuwepo kwa matumizi ya kategoria za kileksika tofauti katika ujengaji wa sentensi za makundi mawili haya kunapelekea kukosekana kwa mawasiliano fanisi miongoni mwa wazungumzaji wa Kiswahili. Data za utafiti huu ambazo kwa kiasi kikubwa zilikusanywa kwa njia ya mahojiano au ushuhudiaji zinadhihirisha kuwepo kwa

matumizi ya kategoria za kileksika zinazotofautiana. Sentensi za lahaja ya Kipemba zifuatazo hapa chini zinashadidia hoja hii;

i) *Ngwiye* guu (KP)
Mkamate mguu (KS)

ii) Kun'nitilia viziwa *vihibi* (KP)
Umenitilia maziwa kidogo (KS)

iii) Bukule *lin'geleka* (KP)
Daftari lake limepotea (KS)

iv) Kan'fiswa sukuli ni *mvyelewe* (KP)
Amepelekwa shule na mzazi wake (KS)

v) Kisuche nakipachika apo *kizani* (KP)
Nimekipachika kisu chake hapo kiambazani (KS)

Sentensi za hapo juu zimejengwa na kategoria za kileksika ambazo hazifanani katika sentensi za Kiswahili sanifu na sentensi za lahaja ya Kipemba. Licha ya tofauti hizo za kikategoria za kileksika, ujembe (taarifa au maana) za sentensi hizo ni ile ile. Maneno 'ngwiye, vihibi, lin'geleka, mvyelewe na kizani' yaliyotumiwa katika lahaja ya Kipemba yanawakilishwa na maneno 'mkamate, kidogo, limepotea, mzazi wake, na kiambazani' (kwa mpangilio) katika Kiswahili sanifu.

#### 4.3.2.2 Muundo wa Kirai Nomino

Tulifafanua hapo awali kuhusu kirai na kisha Kirai Nomino kuwa fungu hili la maneno hutawaliwa na nomino au kiwakilishi ama pekee au vikiambatana na maneno mengine. Miundo ya Kirai Nomino iliyomo kwenye sentensi za Kiswahili sanifu hutofautiana na miundo iliyomo kwenye sentensi za lahaja ya Kipemba. Mfuatano wa maneno yanayotumika katika kuunda kirai hiki haufanani kwani katika lahaja ya Kipemba:

1. Nomino inaweza kutanguliwa na kivumishi. Mfano;

a) Uyo mwanao yuapiga wanangwa (KP)
V N +V T N+KH
Mtoto wako huyo anapiga watoto wa watu (KS)
N V V T N H N

b) Nchukuliye kakeyo ichi chakulache (KP)
T N +(V) V N +(V)
Mchukulie kaka yako chakula chake hiki (KS)
T N V N V V

c) Hii pesaye sebumpa tena (KP)
V N (+V) (Ts)+T E
Pesa yake hii sitampa tena (KS)
N V V T E

2. Kivumishi kinaweza kuunganishwa pamoja na nomino. Mfano;

i) Kitabucho kinchanwa n'nduguyo (KP)
N+(V) T (H)+N (V)

Kitabu chako kimechanwa na mdogo wako (KS)
N V T H N V

ii) Mwalimuwe hekuja (KP)
N+(V) T
Mwalimu wake hakuja (KS)
N V T

b) Mamaye yuaumwa tangu majuzi (KP)
N+(V) T E E
Mama yake anaumwa tangu juzi (KS)
N V T E E

#### 4.3.2.3 Muundo wa Kirai Kitenzi

Muundo wa Kirai Kitenzi hukitwa kwenye kitenzi. Kitenzi kikuu au kitenzi kishirikishi huwa ndilo neno kuu katika Kirai Kitenzi. Vitenzi hivi huweza kutanguliwa na kitenzi kisaidizi. Pia huweza kufuatwa na Kirai Nomino na/au Kirai Kihusishi na/au Kirai Kielelzi. Pamoja na hayo, sentensi za lahaja ya Kipemba hazilizingatii sana jambo hilo na kwamba Kirai Kielezi kinaweza kutokea katika mazingira yoyote iwe kabla, baada au hata kuungana na kitenzi (kirai kitenzi). Pia, kiwakilishi kiulizi huweza kuunganishwa na kitenzi. Mfano;

a) Kwenu warudi saa ngaa? (KP)
E T E E
Unarudi nyumbani saa ngapi (KS)
T E E E

b) Kashakwendavye (KP)
T+(E)
Ameenda nyumbani (KS)
T E

c) Aandikani? (KP)
T +(E)
Anaandika nini?
T E

Ni dhahiri kuwa muundo wa vipashio vijengavyo miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu haifanani mara zote na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa sentensi za lahaja ya Kipemba hujengwa na KN+KT, ambapo haikutofautiana na Kiswahili sanifu. Isipokuwa muundo wa sentensi za lahaja

ya Kipemba mara nyingi katika kikundi nomino hujengwa na maneno mawili yaliyoambikwa pamoja na kuunda neno moja, hivyo hivyo katika KT, KE, n.k. Baadhi ya vipashio vinavyoambikwa pamoja ni kama vile (N+V), (T+E), (E+V), n.k. kwa mfano, Ntotongwa (N+V), Nyumbanikwe (E+V), afanyani (T+E).

Pia katika sentensi za Kipemba king'ong'o cha ufizi /n/ hutumika zaidi badala ya king'ong'o cha midomo /m/. Si hayo tu bali pia Kipemba kina vipashio mbali mbali vinavyowakilisha matumizi ya nafsi ya kwanza umoja. Vipashio vyenyewe ni kama hivi: {hi-}, {ha-}, na {n-}/{ni)}. Pia vipashio vya nafsi ya tatu umoja huwakilishwa na nafsi {ka-} na {a-}. Pamoja na hayo lahaja ya Kipemba ina sifa ya udondoshaji wa baadhi ya vipashio katika maneno kwa kiasi kikubwa. Hali hii inawezekana kuwa wanapunguza wakati mkubwa wa mazungumzo. Tumeona kwa ufupi tofauti hizo katika Kirai Nomino na Kirai Kienzi. Hapa chini tumetaja tofauti za jumla zinazokipambanua Kipemba.

#### 4.3.2.4 Tofauti za Jumla Zinazojitokeza kwenye Vipashio Mbalimbali

**i) Uambikaji wa Maneno kwenye Vikundi vya Maneno**

Mara nyingi Kirai Nomino KN hujengwa na maneno mawili yaliyoambikwa pamoja na kuunda neno moja, hivyo hivyo katika KT, KE, n.k. Baadhi ya vipashio vinavyoambikwa pamoja ni kama vile (N+V), (T+E), (E+V) n.k. kwa mfano; Ntotongwa (N+V), Nyumbanikwe (E+V), afanyani (T+E). Pia katika sentensi za Kipemba hutumika king'ong'o cha ufizi /n/ badala ya king'ong'o cha midomo /m/.

**ii) Matumizi ya Viwakilishi vya Nafsi**

Si hayo tu bali pia Kipemba kina vipashio mbali mbali vinavyowakilisha matumizi ya nafsi ya kwanza umoja [ni-].Vipashio vyenyewe ni kama hivi: {hi-} kwa mfano, hila, hisoma, hicheza n.k. [ha-]; kwa mfano, hacheka hata hagwa shii na {n/i} aumwa ntumbo. Pia vipashio vya nafsi ya tatu umoja huwakilishwa na nafsi [ka-]. Kwa mfano, kan'kugwa, kan'lala, n.k. Pamoja na hayo lahaja ya Kipemba ina sifa ya udondoshaji wa baadhi ya vipashio katika maneno kwa kiasi kikubwa. Aidha katika matumizi ya njeo lahaja ya Kipemba inatumia njeo zifuatazo:

a) Wakati uliopita: Kipemba kinatumia mofu {e-} katika uyakinishi na ukanushi pia badala ya {-li-} na {-ku-} kwenye Kiswahili Sanifu, Kwa mfano; nekwenda, ekuja, ekufa, echeza, n.k. Kwa upande wa ukanushi vitenzi hivyo vitawasilishwa kama sekwenda, sekuja, sekufa, hecheza, n.k.

b) Katika njeo ya wakati uliopo uyakinishi Kipemba hutumia kiambishi {-a-} na kipashio z+(-i) kwenye ukanushi. Mfano wa vitenzi vya Kipemba kwenye njeo hii ni nafa, twalima, ala, n.k kwenye uyakinishi na sifi, hatulimi, hali, n.k. kwenye ukanushi.

c) Wakati timilifu: Katika lahaja ya Kipemba wakati timilifu huwakilishwa na mofu {n(a)} kwenye umbo la kitenzi badala ya {-me-} inayotumika katika Kiswahili sanifu. Kwa mfano kan'kufa, nnasema, kan(a)potea. Kwenje ukanushi Kipemba

hutumia mofu {-ja-}. Mifano ya vitenzi vya Kipemba vinavyotumia njeo hiyo ni hajafa, hajasema, hajapotea, n.k.

### iii) Kugeuzwa kwa Vihusishi au Kutokutumika Kabisa

Licha ya hayo, pia kuna ukakasi wa baadhi ya vihusishi ndani ya sentensi za Kipemba. Kihusishi “na” katika Kiswahili sanifu hujitokeza kama “ni au n” katika Kipemba. Mfano,

a). Asha kan’pigwa n’kakeye (LKP) badala ya Asha amepigwa na kaka yake (KS).

b). Kanpelekwa sukuli ni babaye (LKP) badala ya amepelekwa shule na baba yake (KS)

Pia, matumizi ya kihusishi “katika” si makubwa au hakitumiki kabisa na badala yake kihusishi “kwenye” ambacho katika Kipemba hutamkwa “kwene” au “pene” au “mwene” n.k kutegemea na upatanisho wa kisarufi ndivyo hutumika zaidi. Mfano;

a). Kwene nkutano kwena mijitu (LKP) badala ya Katika mkutano kulikuwa na watu wengi (KS),

b). Pene fujo usende (LKP) badala ya penye fujo usende (KS) n.k.

### iv) Matumizi ya Mofu Tofauti Kwenye Eneo Moja au Mazingira ya Aina Moja

Pia Kipemba kinatumia mofu zaidi ya moja ya wakati timilifu wa tendo, kinatumia mofu {-n-}, {-ma-} na {-na-} badala ya {-me-}. Kwa mfano, kan’kugwa (KP) maana yake ameanguka (KS), kamaiba (KP) maana yake ameiba (KS), kanampiga (KP) maana yake amempiga (KS).

#### v) Matumizi ya Viangami

Hali hii inajitokeza kwenye aina zote za sentensi na katika hali karibu zote za kueleza, kukanusha, kuuliza na kuamrisha. Pia, maneno mengi yanapokea sifa hii ingawa hujitokeza sana katika nomino. Mfano; (a) Nkwewe (KP) badala ya Mkwe wake (KS), (b) Nyumbaye (KP) badala ya Nyumba yake (KS), (c) Halivijipika (KP) badala ya Hajui kupika (KS), (d) Kantumwa n'babaye (KP) badala ya ametumwa na baba yake (KS), n.k.

## 4.4 Athari za Kimawasiliano Zinazotokana na Tofauti Baina ya Miundo ya Sentensi za Kiswahili Sanifu na Miundo ya Sentensi za Lahaja ya Kipemba

Data za utafiti huu zimebainisha kuwepo kwa tofauti baina ya miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu na sentensi za lahaja ya Kipemba. Tumezieleza tofauti hizo kuwa ni pamoja na kategoria za kileksika, muundo wa kirai nomino, muundo wa kirai kitenzi, matumizi ya viangami katika sentensi za lahaja ya Kipemba, matumizi ya mofu mbalimbali zinazoambikwa kwenye aina za maneno, n.k. Tofauti hizi huchangia kukosekana kwa mawasiliano fanisi baina ya wazungumzaji mbalimbali wa Kiswahili kunakosababishwa na;

### 4.4.1 Kukosekana kwa Maelewano Baina ya Wazungumzaji

Kutoelewana (kabisa) baina ya wazungumzaji wa makundi haya mawili ya sentensi (watumiaji wa sentensi za Kiswahili sanifu na wazungumzaji wa sentensi za lahaja ya Kipemba) ni athari mojawapo. Hali hii hujitokeza kutokana na matumizi ya kategoria za kileksika zinazotumika upande mmoja tu (katika sentensi za lahaja ya Kipemba) ambapo kwa watumiaji wa sentensi za Kiswahili sanifu hushindwa kutambua ujumbe

au maana inayowasilishwa na misamiati hiyo. Maneno kadhaa yatumiwayo katika sentensi za lahaja ya Kipemba hayapatikani katika kamusi la Kiswahili sanifu kutokana na kutokuwa sanifu hivyo watumiaji wa Kiswahili sanifu hushindwa kutambua maana zake. Mfano wa maneno hayo ni haya yaliyotumiwa katika sentensi zifuatazo;

i) Kakeye *kankugwashi* (KP)
Kaka yake ameanguka chini (KS)

ii) Mameye *hebu* mihogo ya kupwaza (KP)
Mama yake hataki (kula) muhogo uliochemshwa (KS)

iii) *Wan'gwiya* jivi (KP)
Wamemkamata mwizi (KS)

iv) Izo *ndaza kazigele* (KP)
(Nenda) ukazitupe taka hizo (KS)

v) Uyo kukuwo *kakuta magi* mangaa (KP)
Kuku wako huyo ametaga mayai mangapi? (KS)

### 4.4.2 Kuelewana Vibaya Baina ya Wazungumzaji

Kupotoshwa kwa ujumbe baina ya wazungumzaji wa makundi haya mawili ya sentensi (watumiaji wa sentensi za Kiswahili sanifu na wasemaji wa sentensi za lahaja ya Kipemba) ni hoja nyingine. Hali hii hujitokeza kutokana na matumizi ya maneno au miundo yenye kufanana katika pande zote mbili ambapo kwa watumiaji wa sentensi za Kiswahili sanifu hubeba maana (ujumbe) tofauti na ule unaokusudiwa na wazungumzaji wa sentensi za lahaja ya Kipemba. Hali hii husababibishwa na matumizi ya maneno au vifungu vya maneno vinavyotumika katika pande zote mbili ingawa maana za vifungu hivyo vya maneno hutofautiana miongoni mwa watumiaji wa pande hizo. Sentensi zifuatazo zinashadidia maelezo haya;

i) *Kamuuze* kakeyo (KP)

(Nenda) ukamuulize kaka yako (KS)

ii) Miye ta *siji* (KP)
Mimi sijui hata (KS)

iii) Karibu *ukale* (KP)
Karibu ukae (KS)

iv) *Chunga* ng'ombeyo (KP)
Chukua hadhari na ng'ombe wako (KS)

v) Kumbe *wacha wavyeleo*? (KP)
Kumbe unawaogopa wazazi wako? (KS)

Ukichunguza kwa makini sentensi za hapo juu utabaini kuwa sentensi za lahaja ya Kipemba zimetumia maneno au vifungu vya maneno vyenye taarifa inayoweza kupokewa tofauti baina ya msikilizaji anayetumia Kiswahili sanifu na msikilizaji anayetumia lahaja ya Kipemba. Maneno 'kamuuze, siji, ukale, chunga na wacha yanaweza kueleweka kwa maana ya 'kuuza, kutokuja, kula, kuelekeza na kuacha (kwa mpangilio) tofauti na maana iliyokusudiwa na msemaji kwa Kiswahili cha lahaja ya Kipemba.

**4.5 Mjadala wa Matokeo ya Utafiti**

Utafiti huu ulikuwa na malengo makuu matatu, lengo la kwanza lilikuwa ni kubaini miundo ya sentensi za Kiswahili Sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba. Lengo hili liliibuwa swali la utafiti lisemalo kwamba miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu na Miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba ikoje? Mtafiti katika kujibu swali hili aligundua kwamba, miundo ya sentensi za Kiswahili Sanifu na za lahaja ya

Kipemba ni ya aina tatu, sahili, changamani na ambatani na kwamba kila aina ina muundo zaidi ya mmoja.

Katika lengo la pili lisemalo kwamba kubaini tofauti baina ya miundo ya sentensi za Kiswahili Sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba, mtafiti ameongozwa na swali lisemalo kwamba "ni zipi tofauti baina ya miundo ya sentensi za Kiswahili Sanifu na miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba?" Katika kujibu swali hili mtafiti amegunduwa kwamba lahaja ya Kipemba nacho ina miundo inayolingana kwa kiasi kikubwa na Kiswahili Sanifu. Tofauti ya msingi inajitokeza kwenye vipashio vinavyounda virai ambapo virai vya lahaja ya Kipemba vina sifa kama za uangami, udondoshaji na tofauti za matumizi ya viambishi vya nafsi, njeo na hata baadhi ya katagoria nyingine za maneno kunakozifanya tungo za aina zote kujitofautisha kimuundo na zile za Kiswahili Sanifu.

Lengo la tatu ni kubainisha athari za kimawasiliano zitokanazo na tofauti za miundo ya sentensi baina ya lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu. Mtafiti aliongozwa na swali lisemalo kwamba Kwa jinsi gani mawasiliano fanisi huathiriwa na tofauti za miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu? Mtafiti amebaini kuwa zipo athari zinazojitokeza na kukwamisha mawasiliano fanisi ikiwemo kutoelewana kabisa, na kuelewa tofauti na inavyokusudiwa.

Kwa ujumla matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa hakuna tofauti ya miundo ya sentensi baina ya lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu. Tofauti inajitokeza katika

vipashio vinavyounda virai. Tofauti hii inajitokeza kwenye hatua zote za vipashio kuanzia kwenye muundo wa mofu mpaka kwenye muundo wa sentensi yenyewe. Tofauti ya muundo inatokana na uambikaji na udondoshaji wa maneno kwenye vipashio viundavyo Kirai Nomino na Kirai Kitenzi, uambikaji wa maneno kwenye virai, kukosekana au kubadilika kwa baadhi ya njeo na hasa njeo za wakati. Mabadiliko yote haya yanatokana na tabia ya lahaja ya Kipemba kutumia viangami vinavyopelekea kupunguza na kuunganisha maneno, pamoja na ukakasi utokanao na tofauti ya kileksika na maana za maneno.

Matokeo ya utafiti huu yanaenda sambamba na matokeo ya Juma (2011), Faki (2011) na Abdalla (2012) ambao waligundua kwamba lahaja ya Kipemba ina tofauti na Kiswahili sanifu. Aidha matokeo hayo yalionesha kwamba sentensi za lahaja ya Kipemba zina miundo ambayo inatofautiana na Kiswahili sanifu na kwa kiasi kikubwa sentensi hizo za lahaja ya Kipemba zinakwamisha mawasiliano fanisi kati ya wazungumzaji wa lahaja ya Kipemba na wazungumzaji wa lahaja zingine za Kiswahili ikiwemo Kiswahili sanifu.

Tofauti na tafiti zingine matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa tofauti ya miundo haijitokezi tu kati ya lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu ama lahaja zingine za Kiswahili, bali kuna tofauti ya miundo ya sentensi kati ya wazungumzaji wa eneo moja la lahaja ya Kipemba na eneo lingine. Kwa matokeo haya inawezekana kwamba kuna uwezekano wa kuwepo kwa vilahaja zaidi ndani ya lahaja ya Kipemba. Tofauti kubwa kati ya wazungumzaji wa maeneo mbalimbali ni namna wanavyodondosha na kuunganisha maneno tofauti, tofauti ya njeo za wakati wanazozitumia na msambao

wake na tofauti ya viangami ambavyo ndio msingi wa tofauti (ndiyo tofauti kubwa) kati ya lahaja hii (Kipemba) na Kiswahili sanifu na lahaja zingine za Kiswahili.

Sehemu ya pili ya utafiti huu ambayo inatokana na sehemu iliyopita ilikuwa ikiangalia kama tofauti hizo za miundo ya sentensi za Kipemba na Kiswahili sanifu zinakwamisha mawasiliano fanisi. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa tofauti iliyopo kwenye miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba inaathiri sana mawasiliano fanisi kati ya wazungumzaji wa lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu na kati ya wazungumzaji wa sehemu moja ya lahaja ya Kipemba na sehemu nyingine ingawa kwa viwango tofauti. Wakati wazungumzaji wengine wanaozungumza lahaja ya Kipemba wanaweza kukosa mawasiliano fanisi kwenye baadhi ya maeneo, wazungumzaji wa Kiswahili sanifu wanaweza kukosa mawasiliano kabisa kwenye baadhi ya maeneo ya wazungumzaji wengine wa lahaja ya Kipemba kama ilivyooneshwa katika ugunduzi wa Abdalla (2012) na Faki (2011).

### 4.6 Muhutasari wa Sura

Sura hii iliwasilisha na kujadili matokeo ya utafiti huu. Imebainisha malengo mahususi na kuyafafanua pamoja na kuonesha namna yanavyochangia kufikia lengo la jumla la utafiti huu. Sura hii imeanza na utangulizi, lengo mahususi la kwanza, lengo mahususi la pili, lengo mahususi la tatu na mwisho ni muhutasari wa sura.

## SURA YA TANO

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha hitimisho, na mapendekezo ya utafiti huu kuhusu tofauti za sentensi za lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu zinavyokwamisha mawasiliano fanisi [baina ya wazungumzaji wa Kiswahili]. Hapa tulieleza kwa kifupi malengo, maswali ya utafiti na mbinu za utafiti zilizotumika. Kisha tuliteleza matokeo ya utafiti huu na kutoa hitimisho kutokana na matokeo yenye uhusiano na malengo na maswali ya utafiti huu. Mwisho tutatoa mapendkezo yenye uhusiano na mada ya utafiti huu.

### 5.2 Hitimisho la Utafiti

Utafiti huu ulikusudia kuchunguza tofauti za sentensi za lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu zinavyokwamisha mawasiliano fanisi baina ya wazungumzaji wa Kiswahili. Hivyo,utafiti huu ulichunguza tofauti baina ya miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba na miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu. Pia ulijihusisha na ulinganishaji wa lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu kwa lengo la kubaini namna mawasiliano fanisi yanavyowezekana au kukosekana baina ya wazungumzaji wa lugha ileile ingawa wanaiongea katika maeneo tofauti.

Katika kujibu maswali ya utafiti kuhusiana na lengo la kwanza la utafiti huu, tulilazimika kukusanya sentensi mbalimbali zitumikazo katika jamii ya *Wapemba* ambao lahaja ya Kipemba ndiyo nyenzo yao kuu ya mawasiliano. Jicho letu lilitazama zaidi maeneo ambayo hayajapokea athari za usasa na maendeleo ya sayansi na tekonolojia. Maeneo ya vijijini ndiyo tumeyapa nafasi kubwa katika ukusanyaji wa

data. Pia tulikusanya sentensi za Kiswahili sanifu zinazotumiwa na Wapemba wa maeneo ya mjini.

Matokeo ya utafiti yalionyesha kwamba hakuna tofauti ya miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu isipokuwa kuna tofauti ya vipashio vinavyounda virai katika sentensi za Kipemba. Aidha ugunduzi wa utafiti huu umeonyesha kuwa tofauti hiyo ya vipashio vinavyounda virai ndivyo vinavyosababisha kukosekana kwa mawasiliano fanisi.

Kwa matokeo hayo utafiti huu unahitimisha kwamba licha ya kuwa hakuna tofauti ya miundo ya sentensi za lahaja ya Kipemba na sentensi za Kiswahili Sanifu, hata hivyo kuna tofauti ya vipashio vinavyounda virai kati ya sentensi za lahaja ya Kipemba na sentensi za Kiswahili Sanifu ambavyo vinakwamisha mawasiliano fanisi.

## 5.3 Mchango wa Utafiti Huu

Kazi hii ni nyongeza ya kazi zilizotumia nadharia ya makutano na mwachano na nadharia ya Sarufi Miundo Virai. Ni miongoni mwa kazi zilizojihusisha na utafiti kuhusu lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu. Kazi hii inatoa mchango mkubwa kwa wanaisimu miundo. Tunaamini kuwa mbinu tuliyoitumia katika kuchunguza miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu na lahaja ya Kipemba pia zinaweza kutumika katika kuchunguza vipashio vidogo zaidi kama vile vishazi, virai, maneno na mofu. Matokeo ya utafiti huu yamesaidia kubainisha athari za tofauti za miundo ya sentensi baina ya watumiaji wa lahaja mbili tofauti za lugha moja.

Kazi hii imeweza kubaini kuwa vipashio vya kisarufi vinavyobainika katika lugha mbalimbali hujitokeza kwa namna tofauti katika lahaja za lugha moja. Ingawa lugha zinaweza kulinganishwa na kubainika zinafanana kimuundo, tofauti ndani ya lugha moja zinaweza kujitokeza kama data za utafiti huu zilivyobainisha. Pamoja na mfanano wa miundo ya juu (sentensi) ya lahaja mbili au zaidi, tofauti za mpangilio na idadi ya vipashio vinavyojenga miundo hiyo zinaweza kujitokeza kama matokeo ya utafiti huu yalivyothibitisha.

Mwisho, utafiti huu ni nyongeza ya tafiti zinazojadili na kuthibitisha dosari za sarufi mapokeo na haja ya matumizi ya mbinu za kiisimu katika uchunguzi wa lugha. Madai ya wanasarufi mapokeo ya kuchunguza lugha mbili au zaidi kwa kutumia mbinu, miundo, vipashio na dhana zingine za lugha moja [kwa mfano; kuchunguza lahaja za Kiswahili kwa kutumia mbinu na misingi ya Kiswahili sanifu] yanapingwa vikali na matokeo ya utafiti huu. Tumeona jinsi lahaja ya Kipemba inavyojipambanua pindi ikilinganishwa na Kiswahili sanifu. Viangami na udondoshaji ni michakato muhimu ibainikayo kwenye lahaja ya Kipemba zaidi na pengine haitumiki kabisa katika Kiswahili sanifu.

**5.4 Mapendekezo Kuhusu Tafiti za Baadaye**

Utafiti huu umebaini kuwa eneo kuhusu lahaja linahitaji kuchunguzwa kwa kina. Eneo hili bado halijashughulikiwa ipasavyo. Kuna hazina kubwa iliyofichika ndani ya lahaja za Kiswahili. Kilichogundulika baada ya utafiti huu ni kuwa lahaja ni sehemu muhimu sana ya lugha sanifu. Hazina ya kimuundo pamoja na kategoria za kileksika

vikichunguzwa ipasavyo vinaweza kuipa lugha (Kiswahili) sanifu utajiri mkubwa sana. Hivyo, ni vyema kwa watafiti wajao wajihusishe na uchunguzi wa kina kuhusu vipashio vya kimuundo vya lahaja za Kiswahili Kipemba kikiwemo.

Kwa vile imebainika kwamba kuna tofauti ya vipashio vinaunda virai kati ya sentensi za lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu na kwamba vipashio hivyo ndivyo vinavyokwamisha mawasiliano fanisi utafiti huu unapendekeza kwamba tafiti zaidi zifanywe kuchunguza athari za vipashio vinavyounda virai na miundo yake jinsi vinavyokwamisha mawasiliano fanisi. Aidha tafiti zijazo zijikite kuangalia jinsi maneno na miundo yake na mofu; ambazo ndio msingi wa muundo wa neno zinavyokwamisha mawasiliano fanisi. .

## 5.5 Muhutasari wa Sura

Sura hii ilitoa majumuisho kuhusiana na utafiti huu. Inaeleza kwa muhutasari matokeo ya utafiti huu pamoja na muundo mzima wa tasnifu. Baadhi ya vipengele vya sura hii ni hitimisho, mchango wa utafiti huu na mapendekezo kuhusu tafiti za baadaye.

# MAREJEO


Adam, J and Kamuzora, F. (2008), Research Methods for Business and Social Studies, Mzumbe Book Project, Morogoro.

Akmajian, A. and Heny, F., (1975), *An Introduction to the Principles of Transformational Syntax*, M. I. T. Press.

Andrews, R (2003), Research Questions Continuum, London.

Baker, C. L., (1995), *English Syntax,* Massachussets: The MIT Cambridge.

Besha, R. M., (1994), *Utangulizi wa Lugha na Isimu,* Dar es Salaam: Macmillan Aidan Ltd.

Burton-Roberts, N., (1986), Analysing *Sentences*, Longman.

Chomsky, N. (1986), Knowledge *of Language,* Praeger.

Enon, J.C. (1998), Educational Research Statistics and Measurement. Kampala Department of Distance Learning: Makerere University.

Habwe, J. & Karanja, P. (2004), *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*, Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Horrocks, G. (1987), Generative *Grammar*, Longmans.

Huddleston, R. (1984), *An Introduction to the Grammar of English,* Cambridge University Press.

Juma, M.A. (2011), Ulinganishaji wa Lahaja ya Kimakunduchi, Kimtende, Kibwejuu na Kizimkazi. M.A Dissertation, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kahigi, K. K. (1999), *Structural and Cohesion Dimensions of style, A consideration of some texts*, in Maw (1974) RECALL, Belgium.

Katamba, F. (1993), *Morphology*, London: The Macmillan Press.

Kiango, J. G. (1987), *Swahili Anaphoric Expressions*, The Government and Binding Approach, M. A. Thesis, University of Kansas.

Kihore, Y. M. na wenzie (2003), *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanfu (SAMAKISA), Sekondari na Vyuo*, Dar es Salaam: TUKI.

Khamisi, A. M. (1988), "A Typology of Gaps in Kiswahili Sentences" katika Kiswahili, 55 (1-2): 120-133).

Khamis, A. A. (2011), *Uchambuzi wa Kiswahili Fasaha: Sarufi na Lughawiya*, Zanzibar: Chuo Kikuu cha Elimu Chukwani.

Khamis, A. M. na Kiango, J. G. (2000), *Uchanganuzi wa Sarufi ya Kiswahili,* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Kipacha, A. (2007), *Utangulizi wa Lugha na Isimu*, Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Kipacha, A. (2003), *Lahaja za Kiswahili*, Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

King'ei, K. (2010), *Misingi ya Isimujamii*, Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Kothari, C.R. (2009), Research Methodology, Methods and Techniques, Second Revised Edition, New Age International (P) Ltd: New Delhi.

Lambert H.E. (1958) *Chi –Jomvu and Ki ngare Subdialects of the Mombasa area,*Kampala, east African Swahili committee, Studies in Swahili Dialects) Vol: III

Lambert H.E. (1958) *Chi- chifundi. A dialect of southern Kenya Coast,* Kampala, East Africa Swahili committee.

Maganga, C. (1995) *A study of the Morphophonology of Standard Kiswahili, Kipemba, Kitumbatu and Kimakunduchi*, Unpublished PhD Thesis University of Dar – es Salaam

Massamba, D. P. B. na wenzie (1999), *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA), Sekondari Na Vyuo,* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Massamba, D. P. B. na wenzie (2011), *Isimujamii: Sekondari na Vyuo*, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mdee, J. S. (1988), *Sarufi ya Kiswahili: Sekondari na Vyuo*, Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mohamed, A. M. (1986), *Sarufi Mpya,* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Msanjila na wenzie (2011) *Isimu jamii Misingi na nadhari* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Newmeyer, F. (1983), *Grammatical Theory*: *Its Limits and Possibilities*, Chicago University Press.

Radford, A. (1988) *Transformational Grammar*: *A First Course,* Cambridge University Press.

______________ (1997), *Syntactic Theory and the Structure of English*: A Minimalist Approach, United Kingdom: Cambridge University.

Rubanza, Y. I. (2000), *Sarufi ya Kiswahili: Mtazamo wa Kimuundo*, Dar es Salaam: Open University of Tanzania.

________________ (2003), SARUFI: Mtazamo wa Kimuundo, Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Wesana-Chomi, E. (2001), *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili,* Sebha: Kituo cha Utafiti wa Mitaala ya Kiafrika.

Wesana-Chomi, E. (2013), *Kitangulizi cha Mofolojia ya Kiswahili*, Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Whiteley, W. (1969), *Transitivity in Swahili*.

Whiteley, W. H. (1968), *Some Problems of Transitivity in Swahili, London: SOAS*

**______________**(1967), *The Rise of Kiswahil language*, Washington DC: Center of Linguistics.

## KIAMBATISHO 1

## MWONGOZO WA MASWALI YA HOJAJI KWA WAZEE WA KIPEMBA

**MADA**: ***Tofauti za Sentensi za Lahaja ya Kipemba na Sentensi za Kiswahili Sanifu Zinavyokwamisha Mawasiliano Fanisi [Baina ya wazungumzaji wa Kiswahili]***

Mtafiti …………………………………………………   Tarehe …..........…

- Tunaomba utueleze kwa kifupi kuhusu jina lako, umri wako, kijiji unachoishi, kiwango chako cha elimu na shughuli ufanyayo?
- Tunafanya utafiti kuhusu ***Tofauti za Sentensi za Lahaja ya Kipemba na Sentensi za Kiswahili Sanifu Zinavyokwamisha Mawasiliano Fanisi [Baina ya wazungumzaji wa Kiswahili]***. Tunaomba ushirikiane nasi kwa kutupatia taarifa zifuatazo.

---

1. (a) Wapemba wengi wanazungumza Kiswahili lakini wanatofautiana kutokana na maeneo yao wanayoishi. Tubainishie maeneo ya Pemba unayoamini Kiswahili chao kinatofautiana na Kiswahili cha eneo lingine.

(b) Tuelekeze namna mazungumzo yao yanavyotofautiana baina ya eneo moja na lingine [maneno wanayotofautiana, maana zinazotofautiana, sentensi zinazotofautiana, n.k.]

2. Kiswahili cha mjini hakifanani na Kiswahili cha vijijini. Tubainishie namna wazungumzaji wa mjini (mf. Wete, Chake Chake, n.k.) wanavyotofautiana katika mazungumzo baina yao na watu wa kijiji chako.

3. (a) Ni sentensi zipi zinapozungumzwa na watu wa kijiji chako huwapa ugumu katika kuelewa kwa watu wa vijiji au maeneo mengine ya Pemba?

(b) Toa sababu zinazopelekea hali hiyo katika swali la 3 (a).

4. Maneno haya ungeyasemaje kwa Kiswahili kinachotumiwa katika kijiji chako?

(a) *Hatuthubutu kusema chochote kwa sababu sisi ni wageni hapa*

(b) *Mtoto mdogo sana anapenda kula wali kwa mchuzi wa maharage*

(c) *Watoto wake waliotafutwa jana hawajulikani walipo hadi sasa*

5. Toa maoni yako ya jumla kuhusu tofauti za sentensi za lahaja ya Kipemba na sentensi za Kiswahili sanifu zinavyokwamisha mawasiliano fanisi baina ya wazungumzaji wa Kiswahili.

**************** **Tunakushukuru sana kwa mchango wako** ****************

## KIAMBATISHO 2

## MWONGOZO WA MASWALI YA HOJAJI KWA VIJANA WA KIPEMBA WANAOISHI MAENEO YA MJINI

**MADA**: ***Tofauti za Sentensi za Lahaja ya Kipemba na Sentensi za Kiswahili Sanifu Zinavyokwamisha Mawasiliano Fanisi [Baina ya wazungumzaji wa Kiswahili]***

Mtafiti …………………………………………………  Tarehe …..........…

- Tunaomba utueleze kwa kifupi kuhusu jina lako, umri wako, mtaa unaoishi, kiwango chako cha elimu na shughuli ufanyayo?
- Tunafanya utafiti kuhusu ***Tofauti za Sentensi za Lahaja ya Kipemba na Sentensi za Kiswahili Sanifu Zinavyokwamisha Mawasiliano Fanisi [Baina ya wazungumzaji wa Kiswahili]***. Tunaomba ushirikiane nasi kwa kutupatia taarifa zifuatazo.

---

1. (a) Tubainishie maeneo ya Pemba ambayo unadhani huwezi kuelewa namna wanavyozungumza Kiswahili.

(b) Tuelekeze namna mazungumzo yao yanavyotofautiana na mazungumzo ya eneo lako.

2. (a) Ni sentensi zipi zinazozungumzwa na watu wa mtaa wako huwapa ugumu katika kuelewa kwa watu wa vijiji au maeneo mengine ya Pemba?

(b) Toa sababu zinazopelekea hali hiyo katika swali la 2 (a).

3. (a) Sentensi hizi ungezisemaje kwa Kiswahili kinachotumiwa katika mtaa wako?

i) *Karibu ukale*

ii) *Miye ta siji*

iii) *Chunga ng'ombeyo*

iv) *Kamuuze kakeyo*

v) *Wan'gwiya jivi*

vi) *Uyo kukuwo kakuta magi mangaa?*

vii) *Takupaje bembe yangu nawe hupekeyo?*

viii) *Sukari insoza*

ix) *Nchepewe ndiyo nguoye*

x) *Kanifise kwa n'duka hanunue sukari*

(b) Tubainishie tofauti ulizozigundua baina ya sentensi tulizokutajia katika 3 (a) na sentensi ulizozitaja wewe.

(c) Ni matatizo au athari zipi umeweza kuzibaini kutokana na tofauti ulizozigundua baina ya sentensi tulizokutajia katika 3 (a) na sentensi ulizozitaja wewe?

4. Toa maoni yako ya jumla kuhusu tofauti za sentensi za lahaja ya Kipemba na sentensi za Kiswahili sanifu zinavyokwamisha mawasiliano fanisi baina ya wazungumzaji wa Kiswahili.

**************** **Tunakushukuru sana kwa mchango wako** ****************